SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



UKURASA 4

**ASAKWA** madai kubaka, kulawiti watoto wa familia moja





Nipashe
Jumatatu Machi 28, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580898
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

# Baraza la Vijana laibuka mgogoro KKKT Konde

UKURASA 2



Askofu Dk. Frederick Shoo

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### TIKETI KIELEKTRONIKI KUTUMIKA JULAI

SERIKALI imesema kuanzia Julai mosi, mwaka huu, wamiliki wote wa mabasi yaendayo mikoani watatakiwa kukatisha tiketi kwa njia ya...

UKURASA WA 4

### WAFUNGUKA USHIRIKI MDOGO WANAWAKE KATIKA UONGOZI

WADAU wa haki za wanawake na siasa nchini wamepaza sauti kufuatia wiki iliyopita kikosi kazi cha kuratibu maoni ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa kuripoti kuwa kuna changamoto ya ushiriki...

UKURASA WA 8



### MO DEWJI KUFADHILI MASOMO YA MADAKTARI BINGWA NCHINI

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amempongeza mfanyabiashara Mohamed Dewji, maarufu Mo, kwa kujitoa na kuchangia mambo makubwa kwenye Sekta ya Afya.



## Samia aagiza mawaziri kufanya tathmini mpya kwenye vijiji 975

UKURASA 3

## Wadau 100,000 watoa maoni mabadiliko mtaala wa elimu

UKURASA 2

**MICHEZO** BAHATI AJIVUNIA SAFU YA USHAMBULIAJI BIASHARA UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (katikati), akimkabidhi zawadi Paul Michael wa Chuo cha DIT mmoja wa wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo yao kipitia ufadhili wa programu ya Mo Scholars wakati wa hafla ya kusherehekea mafanikio ya programu hiyo mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mwanzilishi wa Mfuko huo, Mohamed Dewji. HABARI UK. 8. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baraza Vijana laibuka mgogoro KKKT

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BARAZA la Vijana wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania KKKT, Dayosisi ya Konde, limemtupia lawama Mkuu wa kanisa hilo nchini, Askofu Dk. Fredrick Shoo, likidai kuongoza mkutano wa kumwondoa Askofu wa dayosisi hiyo, Dk. Edward Mwaikali, badala ya kutafuta njia sahihi ya kumaliza mgogoro unaofukuta.

Akisoma taarifa ya msimamo wa vijana wa dayosisi hiyo jana, Marko Mahenge, alidai Askofu Dk. Shoo amekuwa sehemu ya kukuza mgogoro huo badala ya kutafuta njia sahihi ya kujadili namna ya kushughulika na jambo hilo ambalo linaendelea kuyumbisha Dayosisi ya Konde.

Alisema kwa muda mrefu vijana walikuwa kimya wakifuatilia mwenendo ya mgogoro huo huku wakitarajia kufanyika kwa hekima na busara katika kushughulikia maridhiano ya kuhamisha makao makuu ya dayosisi hiyo kutoka mjini Tukuyu katika Wilaya ya Rungwe na kupelekwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

"Sisi vijana wa Jimbo hili la Mbeya na maeneo mengine ya dayosisi hii tunapinga vikali uamuzi wa Mkuu wa Kanisa kumwondoa Askofu Mwaikali kwenye kiti chake kwa sababu mkutano uliofanyika Machi 22, katika Usharika wa Uyole ulikuwa batili, tunamtambua Dk. Mwaikali kuwa ndiye askofu wetu na hapa jimboni haondoka wala mchungaji au Mkuu wa Jimbo," alisema Mahenge.

Aidha, Mahenge aliliomba Baraza la Maaskofu wa kanisa hilo nchini kuingilia kati mgogoro huo kwa kuiita halmashauri kuu ya dayosisi na viongozi wengine ili kukubaliana mambo ya kufanya.

Akizungumza wakati wa ibada ya Jumapili katika Kanisa Kuu la Ruanda, yalipo makao makuu ya Dayosisi ya Konde, Mkuu wa Jimbo, Mchungaji Nyibuko Mwambola, alisema Halmashauri Kuu haitambui mkutano ulioitishwa na Askofu Dk. Fredrick Shoo kwa madai kuwa ulikuwa batili.

Alimtupia lawama Askofu Dk. Shoo kama mkuu wa kanisa kwa kushindwa kusuluhisha mgogoro huo na kuwa sehemu ya kuchochea hali ambayo alidai inazidi kuongeza chuki na mfarakano.

Kadhalika, alisema baada ya mkutano wa kumchagua askofu mwingine, Geofrey Mwakihaba, Askofu Dk. Shoo alituma waraka kwa taasisi zote za kifedha kufunga akaunti za dayosisi.

Alisema hatua hiyo imewasababishia kushindwa kufanya malipo yoyote ikiwamo mishahara ya wachungaji na watumishi wengine wa dayosisi hiyo.

Vile vile, alidai kuwa Dk. Shoo amewatumia barua wachungaji wote wa Dayosisi ya Konde kuhudhuria kikao kinachofanyika kesho jijini Dodoma, bila kumpa taarifa Askofu wa Jimbo Dk. Mwaikali, na kwamba Halmashauri Kuu imesema naye atashiriki kikao hicho.

"Mkuu wa Kanisa ameonyesha dhahiri upande alipo kwa sababu ameshindwa kutukutanisha pamoja viongozi wa dayosisi na kujadili pamoja namna bora ya kumaliza huu mgogoro badala yake ameonesha wazi kushindwa kusimamia jambo hilo na kuchangia kuchochea suala hili, sisi tunamtambua bado Askofu Mwaikali ndiyo anasimamia dayosisi yetu ya Konde," alisisitiza.

"Haiwezekani Mkuu wa Kanisa aitishe mkutano na kufanya uchaguzi wa kumchagua askofu mwingine, tena kwa siku moja, inaonyesha dhahiri kuna chuki binafsi na sio suala la kuhamisha makao mkuu ya dayosisi."

Machi 22 mwaka huu Mkuu wa Kanisa la KKKT nchini, Askofu Dk Fredrick Shoo, pamoja na wajumbe 201 walifanya mkutano katika Usharika wa Uyole jijini Mbeya kwa lengo la kumaliza mgogoro huo ambapo liliibuka suala la wajumbe kutokuwa na imani na Askofu Dk. Edward Mwaikali.Katika mkutano huo ambao uliendeshwa na Askofu Dk. Shoo na kudumu kwa saa 10, ulitumika kumchagua Askofu mwingine Mchungaji Geofrey Mwakihaba, ambaye alitangazwa mbele ya wajumbe wa mkutano.

Kutokana na uamuzi huo baadhi ya vijana wa KKKT mkoani Mbeya walieleza kuwa mchakato uliotumika kuwa ulikuwa batili.

Hata hivyo, Askofu Dk. Shoo alipotafutwa na Nipashe kwa simu jana, muda wote hakupatikana kuzungumzia suala hilo.

Mgogoro wa kwanini yahamishwe makao makuu ya dayosisi kutoka mjini Tukuyu katika Wilaya ya Rungwe na kwenda Halmashauri ya Jiji la Mbeya, ulianza kufukuta tangu mwaka 2017 hadi sasa.

# ... Mitaala kwa vituo vya 'Daycare' yaja

**Na Mary Geofrey**

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, imesema inakamilisha mtaala wa vituo vya kulelea watoto maarufu 'Daycare'.

Awali vituo hivyo vilikuwa vinatoa elimu na malezi kwa kufuata mitaala ya nje ya nchi na wengine kuviendesha kiholela.

Kamishna Msaidizi wa Ustawi wa Jamii kutoka wizara hiyo, Baraka Makona, aliyaeleza hayo wakati akizindua Chama cha Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo Mkoa wa Dar es Salaam juzi.

"Tupo kwenye hatua za mwisho za kukamilisha mtaala ambao utaanza kutumika nchi nzima, kuanzia mwezi Mei mwaka huu uanze kufanya kazi," alisema Makona.

Alifafanua kuwa, baada ya kukamilika mtaala huo, watafanya kampeni ya kuhamasisha wazazi wenye watoto chini ya miaka mitano wanaenda kwenye vituo hivyo ili kuandaliwa kwa ajili ya kuanza safari ya elimu.

Alisema nchini kuna vituo vya kulelea watoto 6,000 na kati ya hivyo 3,000 vipo Dar es Salaam. Aliupongeza Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuanzisha umoja huo ambao upo pekee nchi nzima na kuitaka mikoa mingine kuanzisha ili kupata umoja wa kitaifa.

"Endeleeni kufanya maboresho ya vituo vyenu ili watoto wasome katika mazingira salama. Wazazi waleteni watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano wafundishwe namna bora ya kuwa wanafunzi wenye uwezo mzuri na maadili mema ya malezi," alisema.

Naye Mwenyekiti wa chama hicho, Shukuru Mwakasege, alisema lengo kubwa la chama hicho ni kutoa elimu kwa wamiliki wa vituo vya kulelea watoto wajue sifa zinazotakiwa kabla ya kuanzisha na kuwalea katika maadili mema.

# Wadau 100,000 watoa maoni mabadiliko mtaala wa elimu

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema hadi sasa, imekusanya maoni takribani 100,000 kutoka kwa wadau wa elimu, kuhusu namna ya kuufanyia mabadiliko mtaala wa elimu nchini, kuendana na mahitaji, mazingira na ushindani wa soko la ajira.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, aliyetoa taarifa hiyo mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam, wakati akizindua bweni la wasichana katika Shule ya Sekondari Loyola.

Alisema mchakato wa ukisanyaji maoni hayo unaendelea kupitia mikutano tofauti kwenye mikoa na kwamba mwishoni mwa mwezi huu, ni zamu ya viongozi wa dini kutoa maoni yao na kisha kufanyika uchambuzi.

Awali Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo, alisema changamoto kubwa iliyopo miongoni mwa wahitimu ngazi ya chuo kikuu, ni kukosa mbinu za mawasiliano na kujiamin i katika uwasilishaji hoja.

"Changamoto zinazowakumba wahitimu ni mbinu za mawasiliano na uwasilishaji, jambo ambalo analo.

Hili kwenye elimu yetu tuliangalie mhitimu daraja la juu lazima awe tofauti na daraja la chini kielimu, aonyeshe umahiri hata katika kujieleza na matumizi ya lugha kwa ufasaha.

Juni, mwaka jana, serikali ilitangaza kufanyia mabadiliko ya mtaala wa elimu, kuanzia ngazi ya awaki, msingi, sekondari na elimu ya juu, ikilenga kuondoa mtazamo hasi kwenye jamii kwamba manufaa chanya ya elimu kwa wahitimu, yanachukua muda mrefu.

Ilisema itazingatia maoni yatakayotolewa na wadau kuhusu uboreshaji mitaala ya elimu, itakayojenga ujuzi, maarifa na stadi za kazi na kwamba Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) itaboresha mitaala ikizingatia maarifa kumudu mazingira yaliyoko na ushindani wa soko la ajira na kuwapata wahitimu wabunifu na wenye uwezo wa kujiajiri.

# Samia aagiza tathmini mpya vijiji 975

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

RAIS Samia Suluhu Hassan (pichani), ameiagiza kamati ya mawaziri nane wa kisekta kufanya upya tathmini juu ya hatima ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kwenye vijiji 975 nchini.

Aidha, ameagiza uchambuzi wa vijiji na mitaa 67 yenye migogoro iliyoko mkoa wa Morogoro, kwa kuangalia mipaka na kuweka sawa, huku vijiji na mitaa 14 vikikusudiwa kufanyiwa upya tathmini ya kina kuona hatua stahiki za kuchukua.

Ameagiza kuwa yote yanapaswa kufanywa kwa kuzingatia yaliyokwisha amuliwa kwenye Baraza la Mawaziri la 2019/2020 na 2021/2022, lengo ni kuzingatia maslahi ya taifa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri nane wa kisekta ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, alitoa taarifa hiyo alipokutana na viongozi na watendaji wa mkoa na wilaya na kubainisha migogoro kwenye mapori ya akiba, vyanzo vya maji, hifadhi, maeneo ya ulinzi, mashamba pamoja na ranchi za taifa.

Alisema maagizo hayo ya Rais yameanza kufanyiwa kazi na kamati hiyo baada ya kupita muda mrefu wa utekelezaji, na kwamba wametakiwa kuhakikisha migogoro hiyo inatatuliwa bila kuzusha taharuki kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo.

Aidha, alisema Septemba 23, mwaka jana walipokutana na Baraza la Mawaziri waliona kati ya vijiji 975 vyenye migogoro, 920 vibaki kwa kusogeza au kupunguza mipaka.

Mabula alisema katika migogoro yote ilionekana migogoro katika vijiji 55 iendelee kufanyiwa kazi zaidi kwa kina.

"Kamati tayari ilifanya uchambuzi zaidi wa migogoro ikiwamo kupokea taarifa mbalimbali kutoka ofisi ya wakuu wa mikoa Tanzania bara, wabunge na taarifa za taasisi na wananchi mmoja mmoja walioiandikia barua wizara,"alisema Waziri Mabula.

Mwenyekiti huyo alisema uchambuzi waliofanya ulibaini kuwa yapo maeneo yaliyohifadhiwa 680 yaliyoko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii yenye migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 vyenye migogoro, huku migogoro 81 kati yake ni ya Morogoro pekee.

Aidha, Waziri huyo wa Ardhi alizitaka taasisi kutambua kuwa wana jukumu la kulinda maeneo yao ya ardhi yasivamiwe na wananchi hasa kama tayari wana hati halali kumiliki maeneo hayo, ikiwamo kuweka alama za kudumu na zinazoonekana katika mipaka ya maeneo yote na kwamba jukumu la kulinda ardhi hiyo siyo la wizara yoyote ile.



"Kuna malalamiko mengi ya taasisi kama shule, JWTZ, Magereza kulalamikia maeneo yao kuvamiwa, kuanzia sasa wekeni vizuri mipaka yenu na ifahamike, hatutarajii tena migogoro, hatutarajii mje kulalamika, wekeni vizuri mipaka yenu na ifahamike vyema," alisema.

Pia alionyesha kukerwa na tabia ya baadhi ya wananchi kuvamia maeneo yasiyoendelezwa ambayo serikali ilishayafutia umiliki wake, huku serikali na viongozi wakiwapo hadi ngazi za chini, na badala yake kutaka viongozi kuingilia kati.

Kuhusu Mkoa wa Morogoro, Waziri Mabula alikiri kuna changamoto nyingi zinazosababishwa na mwingiliano wa matumizi ya ardhi, lakini tayari imefanyiwa kazi na hatua mbalimbali zimechukuliwa ili kumaliza migogoro hiyo.

Akawataka viongozi wa mkoa wa Morogoro kwa kushirikiana na ofisi ya Kamishna wa Ardhi, kuendelea kuainisha maeneo mengine yenye migogoro ambayo hayajaainishwa katika migogoro inayofanyiwa kazi.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shighela, alipongeza uamuzi huo wa Rais ikizingatiwa Morogoro ni miongoni mwa waathirika wa migogoro ya ardhi kwa muda mrefu.

Kamati hiyo inahusisha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maji, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Kilimo, Ofisi ya Rais Muungano na Mazingira pamoja na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).


WIZARA YA ARDHI,NYUMBA NA MAKAZI
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MASWA.

MAHALI MASWA.

MAOMBI MAKUBWA NA.49 YA MWAKA 2021

KATI YA
WILSON LUCAS ...............MWOMBAJI
DHIDI YA
1.SIGWA LUCHIBULA
2.THOMAS EZEKIEL ............WAJIBU MAOMBI

WITO/TAARIFA

Kwa: THOMAS EZEKIEL POPOTE ALIPO KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua Maombi dhidi yenu katika Baraza hili la wilaya ya Maswa.Maelezo ya madai yanaweza kupatika hapa Barazani.Unatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wako wa maandishi(WSD)kabla ya tarehe 12.05.2022.
Pia unajulishwa kuwa Maombi haya yamepangwa kutajwa siku ya tarehe 12.05.2022 saa 2;30 asubuhi mbele ya Mhe.J.T.Kaare Mwenyekiti,Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya-Maswa.
Na pia unafahamishwa kuwa iwapo utakadi wito huu na kushindwa kufika siku iliyopangwa,Baraza litalazimika kusikiliza Maombi haya upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.
IMETOLEWA kwa MKONO wangu na MHURI wa Baraza hili leo tarehe 22.03.2022

J.T.KAARE

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MASWA TANZANIA

J.T.KAARE
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA(W)
MASWA



## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JULIETH CHRISTOPHER MASSAWE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 839 DLF - TOYOTA IST.** Chassis namba **NCP1100012611.** Engine namba **1NZD000331.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/122675/2022.**



tigo

## EXPRESSION OF INTEREST – REF. NO. TRBP/01/22

**Introduction**

**MIC Tanzania Public Limited Company associated with its commercial brand Tigo is an innovative telecommunication company in the country, distinguished as a fully-fledged digital lifestyle brand. With over 10 million registered subscribers, MIC Tanzania Public Limited Company directly and indirectly engages with over 300,000 Tanzanians including an extended network of customer service representatives, mobile money merchants, sales agents and business partners.**

### Invitation to apply for MIC Tanzania Public Limited Company Retail Business Partnership

MIC Tanzania Public Limited Company is looking for reputable limited companies in Tanzania to distribute its preferred best-selling products as well as carrying its brand across sales regions in Tanzania (Mainland & Islands). This business partnership is coupled with attractive products mix with the best commission schemes in the market. The interested companies should have a long-term vision to partner and grow with Tigo, the fastest growing Mobile Network Operator in Tanzania.

### General Criteria

i). The expression of interest will be championed by the internal committee.
ii). Detailed expression of interest document can be obtained from our Headquarters (with the address below), and our website and through the link ***"https://www.tigo.co.tz/tender"***.
iii). Time frame to collect detailed expression of interest document is March 28th, 2022 to April 8th, 2022.
iv). Selection criteria will be as per MIC Tanzania Public Limited Company set criteria according to specific strategic plans for each region/district. Criteria include (but not limited to) capital, ability to open outlet, distribution experience, fully and complying "KYA documents" will be considered during selection
v). MIC Tanzania Public Limited Company shall disqualify any applicant because of failure to follow instructions and meet requirements.
vi). MIC Tanzania Public Limited Company reserves the right to waive minor proposition deficiencies that may not be corrected prior to award determination to promote competition in some cases.
vii). Evaluation of applicants will be conducted as per MIC Tanzania Public Limited Company pre-set selection criteria.
viii). Only selected applicants will be contacted, and no reasons shall be provided to unsuccessful applicants.

### How to apply

i). Submit cover letter to express the business partnership interest along with copies of certified "KYA documents" to our head office per address below.
ii). The application form should be filled in clearly to show the strengths of applying company with the intention to grow with MIC Tanzania Public Limited Company in preferred regions and districts.

**Tender Address:**
Managing Director
MIC Tanzania Public Limited Company
DERM Complex, P. O. Box 2929, Plot. No 11, Block 45A, New Bagamoyo Road, Dar-es Salaam.
Attn: "Application for Retail Business Partner

**Submission:** Deadline for submission is 05:00pm East African Time on April 15th, 2022. No tender fee will be charged

216776602



Ofisa wa Bodi ya Maji Bonde la Mto Wami Dar es Salaam, Halima Faraji, akizungumza na kinamama wanaofanya shughuli za kilimo cha mboga katika Bonde la Mto Mzinga Kata ya Mwanagati, Dar es Salaam juzi, wakati wa ziara ya maofisa wa bodi hiyo na wawakilishi wa kampuni ya TBL ya kuelimisha wananchi kutunza mazingira kwenye mito na vyanzo vya maji, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Maji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Adaiwa kubaka, kulawiti watoto wa familia moja

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

JESHI la Polisi mkoani Geita linamtafuta mkazi wa Kijiji cha Bukori (jina limehifadhiwa), kwa tuhuma za kuwabaka na kuwalawiti watoto watatu wa darasa la tatu wa familia moja wa Shule ya Msingi Bukori.

Wanafunzi hao wameumizwa sehemu zao za siri kiasi cha kushindwa kwenda haja.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Henry Mwaibambe, alisema tukio hilo lilitokea katika Kijiji cha Bukori wilayani Geita, alisema uchunguzi wa awali ulibaini kuwa mtuhumiwa huyo (jina limehifadhiwa) ni mwanafamilia hiyo.

Alisema ukatili waliofanyiwa watoto hao ni ndani ya familia na jamii ambao ulibainika baada ya watoto kushindwa kujisaidia aja zote kutokana na maumivu.

"Ukatili mbaya sana upo ndani ya familia, kuna kesi pale Bukori upelelezi bado unaendelea, ndani ya familia kuna mtu mfanyabiashara sijui yuko wapi, kila akija anawaingilia watoto na kuwaambia wasiseme, na kwenye familia hiyo mtuhumiwa huyo yeye ndiye mwenye uwezo wa kifedha anawapatia fedha za chumvi," alisema na kuongeza:

"Kuna watoto watatu anawafanyia ukatili wa kingono, siku ya kugundulika kwa tukio hilo mwanafunzi mmoja aliingia chooni kujisaidia katika Shule ya Msingi Bukori akashindwa kutoka kwa kuwa sehemu ya haja kubwa ilikuwa imeharibika na wanafunzi wenzake walikuwa wakipiga kelele mbona hautoki chooni ili waingie, hadi mwalimu alipofika akaingia akakuta mwanafunzi huyo akiwa kwenye maumivu makali."

Alisema: "Mwalimu alimpeleka mwanafunzi huyo Kituo cha Afya Bukori, alipohojiwa alimtaja anayewafanyia vitendo hivyo ni ndugu yao anayekuja mara kwa mara, alieleza pia siyo peke yake bali kuna wengine wawili wamefanyiwa kama yeye."

Kwa mujibu wa Mwaibambe, ngazi ya familia ndiyo kuna ukatili mwingi, lakini inakuwa ni ngumu kwa polisi kupata taarifa, na kwamba wanaendelea na upelelezi wa tukio hilo ambalo walijua baada ya mwanafunzi huyo kuanguka chooni.

"Kitendo alichokifanya mtuhumiwa huyo ni cha kikatili sana, sisi polisi tunamtafuta kwa sababu ni mwanafamilia tutampata tu na tukimkamata tutampeleka mahakamani, ili sheria iweze kuchukua mkondo wake," alisema na kuongeza:

"Wazazi na walezi jitahidini kuwakagua watoto wenu wa kike na wa kiume ili kugungua kama wamefanyiwa ukatili wa kingono, mnahangaikia na biashara zenu tu pamoja na VIKOBA hamwangalii maendeleo ya watoto wenu."

Aidha, Kamanda Mwaibambe aliwatahadharisha wananchi wa mkoa huo kuwa wamebaini usafiri wa bajaji ni hatarishi kwa kuwa kuna matukio ya ukatili wa kijinsia na uhalifu mwingine.

# Tiketi kielektroniki kutumika Julai

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imesema kuanzia Julai mosi, mwaka huu, wamiliki wote wa mabasi yaendayo mikoani watatakiwa kukatisha tiketi kwa njia ya kielektroniki ikiwa ni utekelezaji wa mikakati ya kuboresha utoaji huduma hizo kwa wananchi.

Akizungumza jijini Dodoma, Katibu Mkuu Uchukuzi, Gabriel Migire, alisema nia ya kuanza utaratibu huo ni pamoja na kudhibiti mapato yanayopatikana kwa njia ya tiketi na kuwarahisishia wamiliki kujua idadi ya tiketi zilizouzwa kwa siku.

"Changamoto zote zilizowasilishwa awali na wadau zimerekebishwa kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) hivyo kukamilika kwa marekebisho haya kutafanya zoezi hilo kuanza mwezi Julai," alisema Migire.

Katibu Mkuu Migire alisema kwa sasa LATRA itaanza na majaribio kwa miezi mitatu ili kujiweka sawa na endapo itabainika kuwepo kwa changamoto ndogo ndogo zitakamilishwa ili Julai huduma hiyo ianze rasmi.

Akieleza faida za mfumo huo kwa abiria Migire alisema ni kutolazimika kwenda stendi au kutafuta wakala kwa kuwa suala hilo atalifanya kwa kutumia simu yake ya kiganjani.

Aliongeza kuwa kwa abiria wasio kuwa na simu janja watapata tiketi hizo kupitia mawakala wa benki ili kuwapunguzia adhaa ya kutafuta mawakala walio katika stendi za mabasi.

Mkurugenzi wa LATRA, Giliard Ngewe, alisema mamlaka itaanza kutoa elimu kuanzia Aprili mosi ili kuwapa abiria uelewa wa namna ya kukata tiketi hizo kwa kuzingatia makundi yote ya jamii.

Ngewe aliongeza kuwa elimu hiyo imeshirikisha taasisi zote muhimu ikiwamo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) ili kufikia watumiaji kwa haraka.

# Wafunguka ushiriki mdogo wa wanawake katika uongozi

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa haki za wanawake na siasa nchini wamepaza sauti kufuatia wiki iliyopita kikosi kazi cha kuratibu maoni ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa kuripoti kuwa kuna changamoto ya ushiriki wa wanawake na makundi maalum katika siasa, demokrasia na uongozi. Akisoma ripoti hiyo kwa Rais Samia Suluhu Hassan katika Ikulu ya jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa kikosi hicho, Prof. Rwekeza Mukandala, alisema ushiriki wa wanawake na makundi maalum katika siasa, demokrasia na uongozi ni mdogo tofauti na malengo ya kitaifa na kimataifa.

Meneja miradi kutoka Taasisi ya Msichana Initiative, Consolata Chikoti, alisema ni kweli kuwa kuna ushiriki mdogo katika masuala ya siasa, lakini watu wanaona tatizo hilo katika ngazi ya juu kama ubunge na uwaziri wanasahau ulipo mzizi wake katika ngazi ya familia, kata na hata udiwani.

"Wanawake hawawezi kushiriki uongozi katika ngazi ya taifa kama huku chini hawashiriki vizuri, kwa mfano ukifanya research ndogo tu kuwa ni wanawake wangapi nchini ni wenyeviti wa vijiji, kata au madiwani utakuta kwa idadi ni ndogo sana na hawawi groomed (kuandaliwa) kutokana na mfumo ikiwamo ukatili wa kijinsia na ukosefu wa rasilimali,"alisema Consolata.

Alisema pia jamii haimwangalii mwanamke kama kiongozi, hivyo hata anapojaribu kujitosa katika masuala ya uongozi haimuungi mkono kama ilivyo kwa wanamume, ila anatumiwa sana katika kichocheo cha mwanamume kupata uongozi kama vile kufanya kampeni, vigeregere.

Naye Janeth John Mkurugenzi wa Taasisi ya Binti Makini alisema mifumo ya kivyama haimpi nafasi mwanamke kushiriki katika siasa kikamilifu, kwa sababu haina imani naye kuwa anaweza kushiriki katika nafasi kubwa za kisiasa.

"Ndani ya vyama wanahisi kuwa mwanamke akipewa nafasi ya kushiriki nafasi kubwa kitaifa anaweza kupoteza kwa imani kuwa nguvu yake ya ushawishi ni ndogo hivyo mifumo ikiwekwa vizuri na kumsaport mwanamke basi ushiriki utakuwa," alisema Janeth.

Vilevile Janeth alisema kuna tatizo la rushwa ya ngono katika vyama, kuwa ili mwanamke achaguliwe kuwania nafasi za juu au kuchaguliwa viti maalum inamlazimu atoe rushwa hiyo, hali inayowafanya wanawake wengi wakae pembeni ili wasidhalilishe utu wao.

Changamoto nyingine alisema kuwa siasa inahitaji fedha na wanawake wengi hali zao za kimaisha zipo chini ukilinganisha na wanaume hivyo kama wanawezeshwa au kujiandaa mapema kiuchumi basi idadi ya ushiriki wao katika siasa na uongozi itaongezeka.

Naye mtaalamu wa masuala ya siasa, Prof. Ernest Mallya, alisema kuwa pamoja na yote kunatakiwa kuwa na uadilifu na teknolojia katika siasa na demockrasia ili kuwavutia wanawake wengi kuingia katika tasnia hiyo.

"Kunatakiwa kuwe na ikazidiwa teknolojia nzuri itakayoweza itakayoweza kubaini kama kuna kuonevu katika masuala ya kupigakura ili kuleta usawa kwa wanawake na wanaume," alisema Prof. Mallya.

Ripoti hiyo ilieleza pia sababu za kuwapo kwa ushiriki mdogo katika makundi hayo kuwani ni changamoto za kimazingira katika shughuli za kisiasa na uwapo wa mfumo dume katika jamii.

Changamoto nyingine kwa mujibu wa ripoti hiyo ni utaratibu wa kuwapata wabunge na madiwani wa viti maalum kwa baadhi ya vyama vya siasa hauzingatii usawa wa kijinsia, na kutokuwapo na mfumo wa kuvitaka vyama vya siasa kuzingatia usawa huo.

Mapendekezo ya kamati hiyo yalikuwa ni kufuatilia mfumo wa ushiriki wa wanawake na makundi maalum katika siasa na vyombo vya uamuzi na kuangalia jinsi vyama vya siasa vinavyoshughulikia usawa wa kijinsia.

# TIC yajivunia kusajili miradi 266

**Na Julieth Mkreri,** KIBAHA



WAZIRI wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (pichani), amesema miradi 266 imesajiliwa katika Kituo cha Uwekezaji (TIC) kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema hayo jana wakati wa hafla ya kukabidhi kiwanja namba moja kitalu B eneo la Kwala, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kwa mwekezaji wa kampuni ya Sino Tan (Kibaha Industrial Park Ltd) kwa ajili ya Kongani ya viwanda.

Akizungumzia mradi huo mkubwa wa kimkakati kwa Afrika Mashariki na Kusini mwa Jangwa la Sahara, alimpongeza Rais kwa kuhakikisha Tanzania inakuwa eneo salama la uwekezaji na mahali pa kuvutia wageni.

Alisema mradi huo ambao utatekelezwa kwa kipindi cha miaka minne, utaanza kwa miaka miwili ya awali na mingine baadaye na ujenzi wake unatarajia kugharimu zaidi ya Dola za Kimarekani 150 ambazo zitawekezwa katika upatikanaji wa ardhi, miundombinu, ujenzi wa viwanda na vifaa vinavyohitajika.

Alisema manufaa ya uwekezaji wa mradi huo ni uhakika wa soko la malighafi, mikataba iliyosainiwa na kampuni ya Sino Tan inayomilikiwa na wawekezaji kutoka China ni mwanzo wa mradi mkubwa utakaoleta manufaa mapana kwa taifa kwa kuwa viwanda vya kuchakata mazao vitajengwa na Watanzania watanufaika na soko.

Manufaa mengine ni ajira za moja kwa moja 100,000, pia wananchi wanatakiwa kutumia fursa ya kujifunza lugha ya Kichina na Watanzania wanatakiwa kutumia fursa hiyo ili wapate kuwa wakarimani ndani na nje ya Tanzania.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara, Prof. Godius Kayarara, alisema upatikanaji wa ardhi ni jambo kubwa kuliko kitu chochote ndiyo maana sheria zinabadilishwa ili ardhi ipatikane haraka na mradi ufanyike kwa haraka.

Alisema mradi huo utakuwa na viwanda 200 vya kutengeneza bidhaa mbalimbali zikiwamo pikipiki.

Mwakilishi wa Sino Tan Kibaha Jansen Huang, alisema mradi ukikamilika watahitaji huduma ya polisi kwa ajili ya usalama na baadhi ya nchi zenye miradi yake ya uwekezaji ni Nigeria, Ethiopia na Uganda na wana marafiki wengi na kuitaja Tanzania kuwa na sera nzuri kuhusu uwekezaji.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge, alisema wanamshukuru Rais kwa kufanya jitihada za kuweka mazingira bora ya uwekezaji nchini na kwenye mkoa kwa kutafuta wawekezaji na kuboresha maisha.

Kunenge alisema mkoa una viwanda 1,453 vikiwamo vikubwa 87.

# Wafugaji wasimamisha kilimo Kwala

**Na Julieth Mkreri,** KIBAHA

BAADHI ya wakazi wa Kijiji cha Kwala Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani wameiomba serikali kusimamia suala la wafugaji kuhama katika kijiji hicho ili waendelee na shughuli za kilimo.

Wakizungumza na Nipashe, walisema wako hatarini kukumbwa na njaa kwa kuwa msimu huu wa kilimo hawajajishughulisha kwa kuhofia mazao yao kuharibiwa na mifugo.

Denis Makusanya alisema wamekuwa wakilima mazao, lakini baadhi ya wafugaji wanalisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima bila hofu.

"Huku kwetu mihogo ndio tulikuwa tunategemea sana, lakini kwa sasa hakuna tena, mifugo imeharibu imekula mazao yetu yote shambani hata mbegu ya mihogo hatuna tena," alisema Denis.

Alieleza kuwa yupo mfugaji maarufu (anamtaja) alishaelezwa na viongozi wa serikali aondoke aende sehemu ya wafugaji, lakini hadi sasa hajatekeleza agizo hilo, na kwamba wapo wafugaji wengine wameshindwa kuondoka kwa sababu yake.

"Wapo watu wametoka mjini na kununua mashamba huku kwa ajili ya kilimo, lakini wamesimama kuendelea na shughuli zao kutokana na hawa wafugaji, huyu (mfugaji huyo maarufu) akiondolewa na wengine wataondoka wengi wako nyuma yake wanamsikiliza," alisema.

Frank Willson aliliambia Nipashe kuwa wamekuwa wakilalamikia suala hilo kwa viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji hadi mkoa, lakini hadi sasa kero yao haijapatiwa ufumbuzi.

Kwa mujibu wa Frank, amesimamisha shughuli za kilimo tangu mwaka jana, baada ya kupata hasara mara kwa mara anapolima, badala yake ameamua kujikita katika uuzaji wa mkaa ili aweze kuendesha maisha.

Naye Ibrahim Lubeta, mjumbe katika kitongoji cha Mahundi, alieleza kuwa mbali na mazao kuharibiwa, wafugaji hao wamekuwa wakiwapiga wakulima.

"Wanaingiza mifugo yao shambani ukiwaambia waiondoe wanasema watachungia wapi, ukijaribu kuitoa isiendelee kuharibu mazao wanakupiga na kukuumiza... ukilalamika kwa uongozi wa juu hakuna utatuzi unaofanyika kwa wakati," alisema.

Hata hivyo aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandis Evarist Ndikilo, aliwahi kufika na kusikiliza malalamiko ya wananchi hao ambapo alitoa maagizo kwa viongozi wa Wilaya na Tarafa ya Ruvu kuhakikisha wafugaji wanaondoka na kuhamia katika maeneo yao, agizo ambalo hata hivyo halijatekelezeka hadi sasa.

Pia alizuia wafugaji kulisha mifugo yao katika bonde la Mto Ruvu ambapo wakulima wengi wanalitumia kwa kilimo cha umwagiliaji agizo ambalo utekelezaji wake bado haujafanyika.

Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, alipoulizwa na Nipashe kuhusiana na malalamiko ya wananchi, hao alisema atashughulikia suala hilo.

Idadi kubwa ya wakazi wa Kijiji cha Kwala inaelezwa kuwa ni wakulima, huku wengine wakitoka katika mikoa mingine kuhamia katika kijiji hicho kwa ajili ya kilimo, lakini wamekwama kutokana na kubughudhiwa na wafugaji.


## MUHIMBILI NATIONAL HOSPITAL

## VACANCY ANNOUNCEMENT

Muhimbili National Hospital (MNH) is a tertiary Specialised and Super Specialist Hospital in Tanzania organized into nine Directorates with bed capacity of 2,178 out of which 1,570 beds are at the Main Upanga Hospital and 608 beds are at Mloganzila facility which is 30 km away from the main Hospital. The Hospital serves between 2,000-3,000 Outpatients and 1,500 – 2,000 Inpatients per day.

In order to achieve its objective the Hospital is looking for a competent and experienced person to fill the position below for 2 years contract (renewable on mutual agreement)

**1.0 CLERK OF WORKS – (2 POSTS)**

**1.1 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. To observe quality of construction in accordance with the contract and assist in preparation of progress reports.
ii. Consider and evaluate Contractor's suggestions and recommendations, discuss with the Project Supervisor and help in making decisions where appropriate
iii. Maintain accurate records of construction works at the construction site in an orderly manner in accordance with procedures.
iv. Review and verify application for payments submitted by the Contractor and submit recommendations on the way forward
v. Assist in reviewing the list of items to be completed or corrected which are Submitted by the contractor for issuance of a Certificate of Substantial Completion.
vi. Provide assistance in final inspection of the work and in reviewing the record documents to be furnished by the contractor upon completion of the work
vii. To perform any other related duties as may be assigned by his/her supervisor.

**1.2 QUALIFICATION AND EXPERIENCE**

Holder of Bachelor Degree in Architecture and must be Registered with Architecture and Quantity Surveyors Registration Board (AQRB) with Minimum of 2 years of working experience

**1.3 RENUMERATION**

Attractive package in accordance with Hospital salary structure.

**2.0 QUANTITY SURVEYOR – (1 POST)**

**2.1 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Assist in establishment and control of projects' cost estimates and quantities
ii. Assist in preparation or review of projects' Bills of Quantities
iii. Assist in ascertaining projects materials
iv. Assist in initial and preliminary budgeting and cost planning of projects
v. Advice on cost effectiveness of design and construction methodology
vi. To perform any other related duties as may be assigned by his/her supervisor.

**2.2 QUALIFICATION AND EXPERIENCE**

Holder of Bachelor Degree in Building Economics/Quantity Surveying or related field and must be Registered with Architecture and Quantity Surveyors Registration Board (AQRB) with Minimum of 2 years experience.

**2.3 RENUMERATION**

Attractive package in accordance with Hospital salary structure.

**3.0 CIVIL ENGINEER – (1 POST)**

**3.1 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Assist in day to day supervision of Works in Hospital Projects
ii. To carry out specified routine technical tasks
iii. Assist in performing duties related to the profession
iv. To perform any other related duties as may be assigned by his/her supervisor.

**3.2 QUALIFICATION AND EXPERIENCE**

Holder of Bachelor Degree in Civil Engineering and must be registered with Engineering Registration Board (ERB) with minimum of 2 years experience.

**3.3 RENUMERATION**

Attractive package in accordance with Hospital salary structure.

**4.0 SYSTEM DEVELOPER – (4 POSTS)**

**4.1 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Actively participate in project scoping, design, development and testing
ii. Studying organizing requirements, conferring with users; studying current HMIS flow, data usage, and work processes, investigating problem areas.
iii. Develop tools and applications by producing clean, efficient code
iv. Automate tasks through appropriate tools and scripting
v. Review and debug code developed internally and by external software vendors
vi. Perform validation and verification testing of the developed software
vii. Collaborate with internal teams and vendors to fix and improve products
viii. Ensure software is up-to-date with the latest technologies
ix. Support the analysis, problem definition, requirements, solution development and proposed solutions to determine foot for purpose.
x. Document and demonstrates solutions by developing documentation, flowcharts, layouts, diagrams, charts, code comments and clear code.
xi. To perform any other related duties as may be assigned by his/her supervisor.

**4.2 QUALIFICATION AND EXPERIENCE**

Holder of Bachelor degree in Software engineering or Computer Science or Information technology or its related field. Applicants demonstrating to have the following knowledge and skills shall have added advantages;

i. Knowledge of trending Health Information Systems and Technologies in the market
ii. Minimum of 2 years working experience in software development
iii. Familiarity with Agile's Scrum development methodologies
iv. Knowledge of selected programming languages (e.g Java, C#, PhP, Python, C++ and the J2EE platform
v. In-depth knowledge of relational databases (eg PostgreSQL, MySQL and NoSQL database (e.g MongoDB)
vi. Familiarity with various operating system (Android, Linux, Mac OS, Windows).
vii. In-depth knowledge of mobile frameworks at the OS level (iOS, Android & windows)
viii. Strong experience with REST API and web services
ix. Problem-solving and follow-through; pragmatic and thorough

**4.3 RENUMERATION**

Attractive package in accordance with Hospital salary structure.

**5.0 SYSTEM ANALYST – (1 POST)**

**5.1 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Deploy, maintain and troubleshoot core business applications, including application servers, associated hardware, endpoints and databases,
ii. Meet and coordinate with internal and external stakeholders to establish project scope, systems goals and requirements,
iii. Develop, analyze, prioritize and organize requirement specifications, data mapping, diagrams and flowcharts for developers and testers to follow,
iv. Translate highly technical specifications into clear non-technical requirements
v. Manage the set-up and configuration of systems,
vi. Define and coordinate the execution of testing procedures and develop test cases to serve the overall quality assurance process,
vii. Provide documentation of all processes and training as needed,
viii. Develop and implement maintenance procedures, monitor systems health, gather system statistics and troubleshoot reported errors and alarms,
ix. Perform design, implementation and upgrades of information systems to meet the business and user needs,
x. Implement best practices for scalability, supportability, ease of maintenance and system performance.
xi. To perform any other related duties as may be assigned by his/her supervisor.

**5.2 QUALIFICATION AND EXPERIENCE**

i. Bachelor's Degree in Computer Science or Information Technology or related field
ii. Minimum of 2 years working experience in health information technologies and system analysis. Applicants demonstrating to have the following knowledge and skills shall have added advantages;
i. Strong computer, hard ware, software and analytical skills
ii. Proven ability to assess business needs and translate them into relevant solutions
iii. Strong understanding and knowledge of the principles and practices associated with database maintenance and administration
iv. Experience installing, configuring, documenting, testing, training and implementing new applications and systems.
v. Working knowledge of a wide variety of programming languages

**5.3 RENUMERATION**

Attractive package in accordance with Hospital salary structure.

**6.0 MODE OF APPLICATION**

Applicants must send application letter attached with certified copies of academic certificates and up-to-date Curriculum Vitae (CV) with three referees with reliable contacts, postal address, e-mail, and mobile numbers to either of the following address:

**Executive Director,**
**Muhimbili National Hospital,**
**P.O.Box 65000,**
**Dar es Salaam.**
**OR**
**Email: hrt@mnh.or.tz**
**Application Deadline: 06th April, 2022.**

216777602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba jipangeni, tunataka kuwaona robo fainali CAF

**WAWAKILISHI** pekee wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, Simba wanatarajia kushuka dimbani Jumapili wiki hii kwenye mechi yao ya mwisho ya hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba yenye pointi saba, itakuwa nyumbani Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuikaribisha US Gendarmerie ya Niger ambayo ina alama tano zinazoifanya kuburuza mkia kwenye Kundi D ambalo pia linazijumuisha Asec Mimosas ya Ivory Coast na RS Berkane ya Morocco.

Katika kundi hilo, Asec Mimosas ambayo ipo kileleni ikiwa na alama tisa Jumapili itakuwa ugenini nchini Morocco kuvaana na RS Berkane yenye alama saba kama Simba, kila timu ikihitaji ushindi ili kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano hayo ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu Afrika baada ya Ligi ya Mabingwa.

Hivyo, ushindi pekee ndiyo utakaoiwezesha Simba kutinga robo fainali bila kuangalia matokeo ya mechi dhidi ya RS Berkane na Asec Mimosas ambayo inahitaji sare tu ili kusonga mbele.

Kwa upande wa Berkane yenyewe inahitaji ushindi ili kujihakikishia nafasi ya kutinga robo fainali, lakini kama ikipoteza na Simba ikapoteza, basi Asec Mimosas na Gendarmerie ndizo zitakazotinga robo fainali.

Kwa ujumla Kundi D, ndilo gumu zaidi katika michuano hii msimu huu, na hadi sasa matokeo ya mechi za mwisho Jumapili wiki hii ndiyo yatakayoamua miamba miwili itakayofuzu robo fainali kutokana na timu zote kuwa na nafasi.

Hivyo, kinachotakiwa kwa Simba ambayo imeingia kambini jana tayari kwa maandalizi ya mechi hiyo, ni makocha kuhakikisha wanafanyia kazi makosa madogo madogo ambayo wamekuwa wakiyafanya katika mechi tano zilizopita za michuano hiyo.

Katika hilo, pia kila mchezaji hana budi kujituma na kutambua kwamba kadrii timu yao inavyosonga mbele katika michuano hiyo, ndivyo ambavyo thamani zao zinaongezeka, hivyo kujiongezea soko lao kwa kutangaza vipaji vyao kwa klabu kubwa nje ya nchi na hatimaye kuweza kubahatika kusajili na kupata maslahi mazuri zaidi.

Kwa namna ambavyo tumeiona Gendarmerie katika michezo iliyopita ya Kundi D, si timu yakuibeza hata kidogo, kwani inaweza kufanya maajabu dakika yoyote kutokana na ubora wao wa safu ya ushambuliaji ikiongozwa na winga hatari anayeongoza kwa kucheka na nyavu, Victorien Adebayor.

Lakini, Gendarmerie ni timu ya kushambulia mwanzo mwisho bila kujali inacheza nyumbani ama ugenini, hivyo benchi la ufundi la Simba linapaswa kuisuka vema safu yake ya ulinzi kuelekea mchezo huo ili kuweza kushinda na hatimaye kufuzu robo fainali.

Katika hilo pia, makosa ambayo yamekuwa yakifanywa na safu ya ushambuliaji ya Simba kwa kushindwa kutumia vema nafasi wanazotengeneza, ni wakati sasa wakufanyia kazi ipasavyo kabla ya mchezo huo.

Kingine ambacho benchi la ufundi la Simba linapaswa kuwaeleza wachezaji ni kuacha kucheza na jukwaa, lakini kufuta utamaduni wao wa kusubiri hadi kipindi cha pili ndiyo waanze kufanya mashambulizi ya kasi.


Hili tumeliona mara nyingi kwa safu ya ushambuliaji ya Simba ikisubiri hadi kipindi cha pili kuanza kushambulia kwa kasi, na wakati mwingine wanakuwa tayari wameshatangulia kufungwa, hivyo mabeki wa timu pinzani kujenga ukuta imara (kupaki basi) jambo ambalo hupata shida kuwafungua. Hivyo, hawana budi kuhakikisha wanaumaliza mchezo 'asubuhi' tu kwa kupata mabao ya haraka, kwani mechi kama hii, kusubiri hadi kipindi cha pili ndipo waanze msako mkali wa bao, inaweza kuwagharimu katika mchezo huo ambao wanachohitaji ni ushindi tu ili kusonga mbele.

Ikumbumbukwe pia katika michuano hii, timu nyingi zinapopata bao la kuongoza, zimekuwa zikitumia kipindi cha pili kupoteza muda na kucheza kwa 'kupaki basi', jambo ambalo Simba inatakiwa kuliepuka kwa kumaliza mchezo kipindi cha kwanza, hivyo kuwafanya wapinzani wao kuwa watumwa.

Tunachotaka kukiona ni bendera ya Tanzania kwa ngazi ya klabu katika soka ikiendelea kupepea na hatimaye msimu ujao kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), na katika hilo, hakuna njia ya mkato zaidi ya kila mpenda soka nchini na Watanzania kwa ujumla kuiombea Simba isonge mbele kwenye michuano hiyo. Simba ikishinda Tanzania imeshinda, tunaitakia maandalizi mema.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Mkandala asitishwe kujiunga Simba, Yanga

**UMEKUWA** sasa ni kama ugonjwa au utamaduni kwa baadhi ya mashabiki wa soka, viongozi na hata makocha kuwatisha wachezaji wa Kitanzania kutoka timu zinazoitwa au kujiita ndogo kujiunga na Klabu za Simba na Yanga.

Tayari baadhi ya wadau wa soka wameshaanza kumtisha kiungo mshambuliaji Cleophace Mkandala kuwa eti asiharakishe kujiunga na timu yoyote ile kubwa iwe Simba au Yanga kwa sababu tu umri wake mdogo.

"Namshauri Mkandala, asiharakishe kwenda kwenye timu kubwa, atulie kwanza. Hizi timu zina upinzani mkubwa, hazina muda wa kumsubiri mchezaji kijana akue kwanza, na siyo yeye tu, nashauri wengine, tamaa hizi kubwa zisiwaponze." Haya ni maneno yaliyosemwa juzi tu kutoka kwa mmoja wa makocha wakubwa tu.

Ukisikiliza, kuangalia na kufuatilia, au hoja zao wanaleta mifano ya baadhi ya wachezaji ambao wametoka kwenye klabu hizo na kujiunga na klabu kubwa na hawakufanya vema. Ni kweli hutokea dunia kote, lakini si kwa wote.

Hata hivyo, wachezaji wengi wa Kitanzania wanaotoka kwenye klabu ndogo na kwenda Simba au Yanga hushindwa kung'aa kutokana na sababu zao binafsi na wala si kwa sababu ya klabu.

Wengi baada ya kupata pesa za usajili, kupata jina na umaarufu, wanabweteka na kuanza kuingia kwenye mambo mengine ambayo hayatakiwi kwa mchezaji, pia kuwa wavivu wa mazoezi.

Kuna mchezaji mmoja wa zamani aliniambia mchezaji kutoka nje ya Simba na Yanga anaposajiliwa na timu hizo anatakiwa afanye mazoezi mara mbili zaidi ya avyokuwa akifanya kwenye timu yake ya awali kwa sababu awali akiwa kwenye timu za chini huwa hakamiwi na anaweza kucheza mpira kirahisi, lakini anapoingia klabu hizo kubwa kila mpira anaogusa anakutana na watu ambao wanamkabili kisawasawa, hivyo lazima awe imara kwa mazoezi, na umakini zaidi, huku akili ikitakiwa kufanya kazi haraka sana. Akasema hicho ndicho kinachowashinda wachezaji wengi. Hili ndilo linalotakiwa lihubiriwe na wadau wa soka, kuwataka kujiandaa kwenda kuwa mchezaji wa timu kubwa, kama vile mwanafunzi wa shule ya msingi anavyotakiwa kuandaliwa kuingia sekondari na si kumtisha kuwa huko sekondari au chuo hakuwezi kwa sababu kuna masomo magumu sana.

Cha kushangaza ni kwamba wakati wanawatisha wachezaji wa Kibongo, Simba na Yanga zinapokea wachezaji kutoka nje ya nchi ambao hawaogopi chochote, na wanaingia na kucheza soka kwa uwezo na mafanikio makubwa.

Vilevile klabu hizo pia zina wachezaji wa Kitanzania ambao nao wana uwezo mkubwa. Kina Feisal Salum, Aishi Manula, Bakari Mwamnyeto, Shomari Kapombe, Mohamed Hussein, Dickson Job, Aboutwalib Mshery, hawa wote hawakuzaliwa Simba wala Yanga, wametoka kwenye timu zingine na wanacheza, tena kwa viwango vikubwa tu, mbona vipaji vyao havikufa? Tena wamejiunga wakiwa vijana wadogo tu.

Mbwana Samatta asingejiunga na Simba leo hii angekuwa hapo alipo? Alijiunga akiwa mdogo sana, je angeogopa kwa sababu kuli-kuwa na 'mafaza' kina Mussa Hassan Mgosi, angekuwa wapi?

Aboubakar Salum 'Sure Boy', baba yake Salum Aboubakar alijiunga na Yanga kutoka Sigara akiwa bado kijana mdogo, ikiwa na mastaa wakubwa, lakini hakujali, alijiamini na akawa staa kuliko mastaa aliowakuta.

Hata Mrisho Ngassa alisajiliwa kutoka Kagera Sugar, akiwa kijana mdogo, akawika kwa miaka mingi sana.

Ulimboka Mwakingwe akiwa bwana mdogo tu, alisajiliwa na Simba akitokea Reli ya Morogoro iliyokuwa imeshuka daraja, kwa namna ya kushangaza kuingia tu kwenye timu hiyo akaibuka kuwa staa mkubwa, mechi ya kwanza tu alimshangaza kila mtu, na akawa mrithi wa Steven Mapunda 'Garincha'.

Kapombe alitokea Polisi Morogoro na kusajiliwa na Simba kwenye kikosi cha pili, lakini alipojaribiwa mechi moja tu ya Ligi Kuu, ikawa ndiyo moja kwa moja hadi leo.

Mpira ni kujiamini na kufuata miiko yake tu basi, siyo kudanganyana kuwa bado mdogo, ina maana watu wanataka wachezaji wajiunge na Simba na Yanga wakiwa wana miaka kuanzia 30? Tuache kuwatisha wachezaji, cha kufanya ni kuwakumbusha kuwa na nidhamu ya mazoezi na kufuta miiko.

Kwa sasa Mkandala anatafutwa na klabu nyingi, asiogope, badala yake aende tu kusajiliwa kwa kiasi anachohitaji, ila anachotakiwa kufanya ni kwamba ajiandae na ushindani wa namba, kwani anachotakiwa kufanya ni mazoezi zaidi ya yale anayofanya Dodoma Jiji, ajitume na kuwa na nidhamu kwani Jiji la Dar es Salaam lina mambo mengi.

TANGAZO

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# TAARIFA KWA UMMA

## UKWELI KUHUSU UWAZI, USAWA NA UZINGATIAJI SHERIA KATIKA ZABUNI YA KANDARASI YA UNUNUZI WA MFUMO WA STEMPU ZA KODI KWA MUJIBU WA SHERIA YA MANUNUZI

**Dar es salaam 25 Machi, 2022:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania imesikitishwa na taarifa za upotoshaji wa makusudi zilizoandikwa na gazeti la **Mwananchi toleo namba 7573** la tarehe **23 Machi, 2022** iliyoandikwa na Mwandishi Alex Malanga ikiwa na kichwa cha habari kisemacho ***"Zabuni ya stempu za kielectroniki yaibua utata "*** na habari nyingine iliyoandikwa na gazeti dada la **Citizen toleo namba 6004** nalo la siku hiyo hiyo na kuandikwa na mwandishi huyo huyo Alex Malanga likiwa na kichwa cha habari ***"New ETS tender not competitive, say manufacturers"*** habari hiyo hiyo ya gazeti la kiingereza ilibebwa na mtandao wa kijamii uitwao **Tanzania business Insight** ikiwa na kichwa cha habari kinachofanana na gazeti la Citizen.

Mamlaka ya Mapato Tanzania inapenda kuweka wazi kuwa habari tajwa hapo juu hazina ukweli wowote na ni za upotoshaji wa makusudi kwa kuwa zinakiuka misingi na miiko ya uandishi unaohitaji mwandishi kupata ukweli wa pande zote mbili hatua ambayo mwandishi husika na wachapishaji hawakulifanya kwa sababu wazijuazo wenyewe.

Ili kuwekewa ukweli sawa, Mamlaka ya Mapato Tanzania inapenda kuwatangazia Umma na wadau kwa ujumla kuwa TRA ilitangaza zabuni ya ununuzi wa mfumo wa stempu za kielectroniki tarehe **16 Februari 2022** kimataifa kwa utaratibu na uwazi kwa mujibu wa sheria ya manunuzi **(PPA)** ili kuhakikisha kuwa wazabuni wote wanapewa fursa sawa kushiriki. Mamlaka ya Mapato Tanzania **(TRA)** ilitoa vigezo vinavyokidhi wazabuni wote (Neutral specifications) kwa ajili ya kutenda haki, usawa kwa wote, ubora na usalama wa hali ya juu wa mfumo ili kupata bei shindani kwa huduma husika. Pamoja na hayo hadidu za rejea (TOR) za vigezo hivyo zilithibitishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA)

Kwa maana hiyo zabuni inaruhusu kila mzabuni kuwa huru kupendekeza technolojia ya mfumo wa stempu utakaokidhi viwango vya juu vya usalama visivyoweza kughushiwa kirahisi ili kuiwezesha serikali kulinda mapato yake pamoja wazalishaji dhidi ya bidhaa zisizokidhi vigezo pamoja na magendo. Zabuni husika pia imetoa muda wa miezi 6 kwa mzabuni atakayeshinda kujipanga na kuanza kufanya kazi ukilinganinisha na miezi 3 aliopewa mzubuni aliyopo sasa ili kutoa muda wa kutosha kujiandaa.

Wakati zabuni hii ikiendelea, na kwa lengo la kuongeza uwazi, mnamo tarehe **8 Machi ,2022,** wazabuni wote wenye nia ambao walikuwa jumla **26,** walialikwa pamoja na mwakilishi wa shirikisho la viwanda nchini (CTI) kupewa ufafanuzi wa pamoja kuhusu zabuni na namna ya kuwasilisha zabuni zao katika mfumo wa PPRA wa TANePs. Wazabuni walipata fursa ya kuuliza maswali kwa uwazi pamoja na kutoa mapendekezo ya maboresho yakinifu kwenye zabuni,

Sambamba na hatua hii wazabuni tarajiwa walipata fursa ya kutembelea viwanda lengwa kuanzia tarehe **19 hadi 22 Machi. 2022** ili kuelewa namna ambayo wanapaswa kufunga mfumo wa ETS viwandani endapo wakishinda.

Aidha Mamlaka ya Mapato Tanzania pia iliweka muda wa siku **45** ambao ni zaidi ya muda wa chini wa kisheria wa siku **21** kwa mujibu wa sheria za manunuzi ili kutoa fursa kwa mzabuni yeyote duniani kushiriki pasipo na kikwazo cha muda.

Hadi sasa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeendelea kupokea maulizo ya ufafanuzi na kujibiwa mara moja ili kutoa fursa sawa kwa kuwa zabuni hii inaendelea kwa kupitia mfumo wa **PPRA** na **TANePs** na inatoa fursa ya uwazi na haki kwa wote kushindana kwa haki bila upendeleo.

Mamlaka ya mapato Tanzania inapenda kuwaomba wazabuni wote tarajiwa kujitokeza na kushiriki zabuni hii kikamilifu pasipo na wasiwasi ndani ya muda na wapuuze habari za upotoshaji zilizotajwa katika taarifa hii ambazo kwa hakika zina lengo hasi.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na;**

**Richard M. Kayombo**
**MKURUGENZI WA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

216777302



Ofisa Mikopo wa Vikundi Vidogo wa Benki ya Biashara ya DCB, Leticia Nyato, akizungumza na wajasiriamali jijini Dar es Salaam jana, wakati wa mahafali ya kwanza ya mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa fedha yaliyotolewa na benki hiyo kupitia asasi yake ya DCB Foundation. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mo Dewji kufadhili masomo ya madaktari bingwa nchini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amempongeza mfanyabiashara Mohamed Dewji, maarufu Mo, kwa kujitoa na kuchangia mambo makubwa kwenye Sekta ya Afya.

Vilevile, amemwomba kusaidia jitihada za serikali kukabiliana na uhaba wa madaktari bingwa wa mishipa ya fahamu, akibainisha kuwa Tanzania ina uhaba mkubwa kwenye eneo hilo.

Ummy alitoa pongezi hizo jijini Dar es Salaam wakati wa sherehe ya kutimiza kwa miaka minane ya Taasisi ya Mo Dewji Foundation iliyofanyika juzi usiku.

alisema serikali inatambua mchango na juhudi zinazofanywa na Mo Dewji katika sekta mbalimbali ikiwamo afya.

"Mo Dewji amegharamia watoto 100 wenye tatizo la saratani ya damu kupitia Mfuko wa Tumaini la Mama, lakini ametusaidia vifaa tiba kwa ajili ya watoto njiti.

"Hivyo vifaa vilivyotolewa na Mo vimetusaidia katika kuokoa vichanga," alisifu na kumwomba kuunga mkono juhudi za serikali katika kupata madaktari bingwa wa ubongo na mishipa ya fahamu, akibainisha kuwa kwa sasa Tanzania ina upungufu wa madaktari 584.

Kwa mujibu wa waziri huyo, Tanzania kwa sasa ina madaktari bingwa wa ubongo na mishipa ya fahamu 16, ilhali mahitaji ni kuwa nao 600. Viwango vilivyowekwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) ni daktari mmoja kwa kila watu 100,000.

"Pamoja na mambo mengine yote, tungeomba angalau utusaidie kupata japo wataalamu wawili tu ambao watatusaidia katika masuala ya ubongo na mishipa ya fahamu, maana ukiangalia sisi tuna uhitaji wa madaktari 600, lakini hapa tunao 16 tu.

"Na ukiangalia Tanzania ajali ni nyingi, kila siku watu wanaletwa hospitalini wamepasuka ubongo na mishipa ya fahamu, hivyo tunaomba msaada wako kama hautaathiri bajeti zako.

"Lakini niliongea na Rais Samia, akakubali tuwapeleke wataalamu wetu wakasomee mambo hayo ili tupate wataalamu wengi zaidi na sasa tupo katika kuangalia vyuo watakavyokwenda kusoma," alisema.

Mwanzilishi wa Taasisi ya Mo Dewji, Mo Dewji, alimwahidi Ummy kushirikiana naye zaidi katika Sekta ya Afya ikiwamo kufadhili masomo ya madaktari bingwa wa ubongo na mishipa ya fahamu alioombwa na serikali.

Alisema anafurahia kuona mafanikio ya kielimu ya vijana wa Kitanzania zaidi ya 100 walionufaika na ufadhili wa masomo unaofanywa na taasisi yake kupitia Programu ya Mo Schollars.

Mo Dewji alisema alianzisha taasisi hiyo mwaka 2015, akiwa na ndoto ya kuboresha maisha ya jamii ya Kitanzania, akilenga sekta za afya, maendeleo ya jamii na elimu ili kukabiliana na umaskini nchini.

"Nilipozindua Taasisi ya Mo Dewji, nilianzisha Programu ya Mo Schollars ambayo inafadhili masomo ya elimu ya juu kwa vijana wa Kitanzania ambao hawana uwezo wa kugharamia masomo hayo vyuoni.

"Kwa neema ya Mungu hadi sasa nimetumia zaidi ya Sh. bilioni mbili kugharamia programu hii. Katika mwaka wa kwanza, programu hii ilikuwa na wanafunzi 10 tu, wote kutoka chuo kikuu kimoja - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

"Sasa miaka minane baadaye, tukiwa na vyuo washirika 11, tunawafadhili wanafunzi 115 wanaoendelea na masomo huku tukijivunia wengine 40 waliohitimu.

Katika miaka 10 ijayo, tunatarajia kupanua ufadhili wetu ili kuwafikia wanafunzi 1,000," alifafanua.

Mo Dewji aliwataka wanafunzi wanaofadhiliwa na taasisi hiyo kutokata tamaa na kusoma kwa bidii ili baadaye waje kuwa msaada kwa wengine kama wao walivyosaidiwa.

Mmoja wa wanafunzi wanaofadhiliwa na taasisi hiyo, Nyamasamba Msiwa, aliishukuru taasisi kumfadhili na kupata elimu ya juu kwa kuwa familia yake ni duni, akikiri asingemudu gharama za kupata elimu hiyo.

# Marekani yakabidhi bweni la bil. 1.8/-

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), limekabidhi mabweni mapya ya Shule la Sekondari Loyola mkoani Dar es Salaam yenye thamani ya Dola za Marekani $772,000 (Sh. bilioni 1.8) kupitia mpango wake wa shule na hospitali za nchi za nje utakaohudumia wasichana 400.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari mwishoni mwa wiki na Ubalozi wa Marekani nchini, Mkurugenzi wa USAID, Kate Somvongsiri akiwa ameambatana na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, walihudhuria hafla ya kukata utepe wa bweni hilo.

Alisema ukosefu wa usawa wa kijinsia bado unaendelea Tanzania, licha ya juhudi za serikali na washirika wake, na kwamba uandikishaji wa wavulana na wasichana kwenye shule za msingi ni karibu sawa, lakini viwango vya kumaliza sekondari kwa wasichana vinarudi nyuma.

Somvongsiri alisema ndoa za utotoni, mimba na kutothamini mafanikio ya wasichana ni vikwazo, na kwamba miongoni mwa vijana wa Kitanzania wenye umri kati ya 20-24, moja ya tano wa wasichana na theluthi moja ya wavulana humaliza sekondari.

Aidha, alisema Shule ya Sekondari ya Loyola iliyoko katika kitongoji cha Mabibo Farasi, inalenga kuwasaida watoto wanaoishi katika mazingira magumu ambao familia zao hazina uwezo wa kumudu mahitaji yao ya elimu.

Mkurugenzi huyo alisema lengo kuu la mpango wa USAID ASHA jijini Dar es Salaam ni kuongeza idadi ya vijana wa Kitanzania hasa wasichana waishio katika mazingira magumu kupata elimu bora.

"Ujenzi wa mabweni haya mapya utaongeza uandikishwaji na kubakia wa wasichana waishio katika mazingira magumu shuleni hapa kupunguza athari wanazokabiliana nazo kila siku kwenda na kurudi shuleni," alisema.

Aidha, alisema ili kuhakikisha vijana wanapata elimu bora hutengeneza fursa za kujihusisha na kupata maarifa na ujuzi muhimu, na kwamba wataendeleza ustawi wa muda mrefu huku wakijenga nchi kwa mustakabali wanaoutamani.

"Kwa kukabiliana na changamoto wanazokumbana nazo wakiwa shuleni na kwenye jamii yao, wasichana wa Kitanzania wana uwezo mkubwa wa kumaliza elimu yao, kuwa na afya bora, kupata ajira, na kupunguza umaskini katika jamii," alisema.

# Ugonjwa wa saratani wawekewa mkakati

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAANDISHI wa habari mkaoni Mwanza wametakiwa kuandika habari sahihi zinazohusu ugonjwa wa saratani ili kuepukana na taharuki katika jamii.

Kadhalika, waandishi wametakiwa kuandika habari ambazo zitachochea jamii kujitokeza kupima afya zao mara kwa mara kabla ya ugonjwa huo haujafikia hatua mbaya.

Akizungumza wakati wa mafunzo ya siku moja kwa waandishi hao, Meneja wa Ubia, Uwezeshaji na Mawasiliano wa mradi wa TCCP, Dk. Sarah Maongezi, alisema, tatizo lililoko katika huduma za saratani nchini pamoja na wagonjwa wengi kufika katika hospitali wakiwa katika hatua mbaya kutokana na kukosekana kwa taarifa sahihi kuhusu ugonjwa huo kwa jamii.

Kupitia mradi huo ambao unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa(AFD) na Aga Khan Foundation (AKF) wenye thamani ya Euro milioni 13.3, utaboresha miundombinu na vifaa tiba vya huduma ya saratani.

Aidha, mradi huo utaboreshaji huduma na uhamasishaji wa saratani katika jamii, kuendeleza na kukuza rasilimali watu, kukuza taaluma za matibabu na kudumisha ushirikiano na tafiti kuhusu saratani nchini.

Alisema kutokana na uelewa mdogo katika jamii kuhusu saratani kunachangia wagonjwa wengi kufika hospitali wakiwa katika hatua ya tatu na ya nne.

Aidha, alisema Tanzania bado kuna tatizo la vifaa vya upimaji wa saratani ikiwamo kuuzwa bei ya ghali.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), mashine moja ya upimaji saratani inapaswa kuhudumia watu milioni moja, lakini kwa sasa hapa nchini watu milioni 60 wanatumia mashine saba pekee.

Alisema mradi huo unatarajia kuwanufaisha watu milioni 1.7, wenye matatizo ya ugonjwa wa saratani.

Kwa upande wake, Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza ya Sekou-Toure, Dk. Athanas Ngambakubi, akitoa elimu juu ya saratani alisema kuwa mwaka 2020 inakadiriwa watu milioni 1.1 duniani walipata saratani na kati ya hao 711,429 waliofariki wanatoka Afrika.

Alisema hapa nchini watu 40,464 walipata saratani kati yao 26,945 walifariki kutokana na ugonjwa huo.

Alisema kuwa kuna aina 10 za saratani zinazoongoza nchini na kwamba inayoongoza ni ile ya mlango wa kizazi, matiti, tezi dume, umio, ngozi, tumbo, ini, kibofu cha mkoja, haja kubwa na mapafu.

Kwa upande wake, Daktari bingwa wa magonjwa ya saratani upande wa mionzi, kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando, Dk. Beda Likonda, akifungua mafunzo hayo alisema jamii ikipata takwimu sahihi, elimu, tiba na tiba shufaa inaweza kuleta mabadiliko chanya.

HABARI KITAIFA

## Oppo sasa yaja na simu mpya kisasa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya kutengeneza simu ya Oppo jana, imetangaza kuongeza bidhaa zake kwa kuzindua smartphone mpya aina ya A76 na A96 kwa soko lake nchini.

Awali, kampuni hii ambayo ina zaidi ya miaka mitatu ilikuwa na simu aina mbili tu ambazo ni series A pamoja na reno series.

Akizungumza mkoani Dar es Salaam wakati wa kutangaza kuzindua simu hizo, mwishoni mwa wiki, Meneja Mafunzo wa kampuni ya Oppo Tanzania, Farida Mwangosi, alisema wanajivunia kuingiza matoleo hayo mapya.

"Tunajivunia kwa kuzindua simu mpya na ya kisasa ya A76 na A96, huku tukilenga kuhudumia wateja wa kipato cha kati na cha chini kwa bidhaa zenye ubora na unafuu," alisema Mwagosi.

Alisema simu hizo ni za kisasa na uhakika, wameona ni vyema kuleta bidhaa hizo ili kuwawezesha Watanzania kuendana na ulimwengu wa kidigitali kwa kutumia simu janja zilizo bora.

Mwangosi alisema kuwa Oppo A96 imetengenezwa na kuwa na mwanga mzuri na kava lake sio la kuharibika kirahisi.

"Simu hii hata ukiwa na mikono michafu kama vile mafuta haiachi alama ya vidole na pia ina ram 8 ambazo zinaweza kuzidi mpaka 13 huku ikiwa na memory ya 256GB," alifafanua.

Aliongeza kuwa Oppo A96 ina betri yenye uwezo mkubwa wa 5000mAh uwezo wa chaji ukiwa ni 33W ambao huchaji simu kwa dakika 60 tu na ikajaa kwa asilimia 100.

"Kulingana na teknolojia yake, simu hii ina uwezo wa kutambua jinsi unavyochaji kwa haraka kwa asilimia 80 na baada ya hapo itaanza kuchaji taratibu hadi utakapoitoa kwenye umeme. Hii inaongeza uwezo wa battery kwani haitaweza kuwa chaji zaidi ya uwezo wake," Mwangosi alisema.

Aliongeza kuwa pia mteja anaweza kuongeza ram kwenye simu hizo hadi 5 hivyo kumsaidia mteja kutumia simu bila kuwa na tatizo za kuganda, Oppo A76 ina ram 6+128, inauwezo wa kujiongezea ram 5 juu yaani ukawa na ram 11, huku Oppo A96 ikiwa na ram 8+256 na inateknolojia ya kujiongezea ram hadi ram 13.

"Simu zote hizi zina usalama na uhakika kwa kuwa ina uwezo wa kutambua sura na pale inapotambua kuna sura ambayo sio mmiliki wa simu yenyewe, basi ina uwezo wa kuzuia taarifa yeyote mpya kuonekana," alisema.

# Serikali yapigania wanawake kuendelezwa kiuchumi

**Sabato Kasika**

SERIKALI imewataka wadau kuendelea kushirikiana nayo kwa ajili ya kuwezesha wanawake kiuchumi, kwa kuwa wana mchango mkubwa katika maendeleo ya familia, jamii na taifa kwa ujumla.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, katika hafla ya utoaji tuzo za washindi wa shindano la Malkia wa Nguvu 2022, mkoani Dar es Salaam.

Waziri Gwajima alisema, serikali inaendelea kuwezesha wanawake kwa kuwatengenezea mazingira wezeshi wale ambao wameonyesha jitihada za kujikomboa kiuchumi na kuwataka wadau kuunga mkono juhudi hizo.

"Rais wetu Samia amekuwa akihimiza, nanyi waandaji wa Malkia wa Nguvu mmeonyesha mfano mzuri wa kuunga mkono juhudi za serikali kwa kuanzisha mashindano ambayo yanalenga kuwezesha wanawake," alisema Dk. Gwajima.

Alifafanua kuwa wanawake Tanzania ni takriban asilimia 51.04 huku takwimu za kimataifa zikionyesha kuwa wanawake ni nusu ya watu wote duniani na wamekuwa na mchango mkubwa katika uchumi ambapo kitaifa asilimia 80 ya nguvu kazi ya sekta ya kilimo ni wanawake, na kwamba huzalisha asilimia 60 ya chakula chote hapa nchini.

Aidha, alisema katika kuwezesha wanawake, serikali ya awamu ya aita imechukua hatua mbalimbali za kuboresha kipato na kuwaondolea umaskini kwa kutenga Sh. bilioni 62.68 katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye halmashauri zote nchini.

"Lakini hadi kufikia Juni 30, 2021, Sh. bilioni 53.81 zilikopeshwa kwa vikundi 7,993 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu sawa na asilimia 86, ambapo kati ya fedha hizo Sh. bilioni 28.17 zilitolewa kwa vikundi vya wanawake 4,894 vilivyozalisha ajira 52,428, nchini," alisema.

Aliongeza kuwa kupitia Benki ya Biashara kwenye dirisha la mikopo, jumla ya mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 22.3 imetolewa kwa wanawake wajasiriamali 6,326 kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 katika mikoa 26 ya Tanzania Bara.

Waziri huyo alisema, serikali inaunga mkono juhudi zote zinazofanywa na wadau mbalimbali kwa ajili ya kumkomboa kiuchumi wakiwamo Clouds Media Group CMG) ambao waliandaa shindano la Malkia wa Nguvu.

Awali akimkaribisha Waziri Gwajima, Mkurugenzi wa CMG, Joseph Kusaga alisema, wao wamekuwa utaratibu huo kwa miaka mingi na wanaendelea nao ili kuhakikisha mwanamke wa kitanzania anainuka kiuchumi.

"CMG imekuwa na mchango mkubwa katika kuwainua wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, na tutaendelea kufanya hivyo kadri itakavyowezekana ili kuhakikisha makundi hayo yanatimiza malengo yake," alisema Kusaga.




Meneja mafunzo wa kampuni ya kutengeneza simu ya Oppo Tanzania, Farida Mwangosi (kushoto), akionyesha simu ya smartphone mpya ya Oppo A96 baada ya uzinduzi wake uliofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Meneja Mkazi Oppo, Tanzania Lin Ke. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makandarasi wapewa mbinu kuwa imara

**Na Joseph Mwendapole,** DODOMA

MAKANDARASI nchini wametakiwa kuachana na utitiri wa vyama na badala yake watengeneze chama kimoja kitakachokuwa na nguvu ya kuwasemea shida zao kwa serikali na kwa wateja wao.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Consolata Ngimbwa, wakati akizungumza wakati wa kufunga mafunzo kwa makandarasi wa ndani.

Mafunzo hayo ya siku mbili yalilenga kuwajengea uwezo makandarasi wa ndani kuhusu namna bora ya kutekeleza miradi ya ubia (Joint Ventures) ambapo makandarasi wa mikoa mbalimbali walishiriki.

Aisema inasikitisha kuona kila kukicha vinaanzishwa vyama vya makandarasi ambavyo havina nguvu badala ya kuanzisha kimoja kitakachokuwa na sauti kubwa ya kuwapambania kwenye shida.

"Kadri siku zinavyozidi kwenda vyama vinazidi kuzaliwa mpaka wakati mwingine nakaa najiuliza tumekuwaje tunashindwa na hata watu wa bodaboda, tukihamasishana wengine wanazalisha chama kingine."

Alisema utafika wakati ambapo makandarasi watapata matatizo ambayo watahitaji kusaidiwa na chama kimoja lakini kutokana na ubinafsi ulioko watabaki wanashangaana wasijue cha kufanya.

Alitoa mfano kuwa Misri walikuwa na vyama vingi vya makandarasi lakini serikali iliingilia kati na kuwasaidia kuanzisha chama kimoja chenye nguvu ambacho kinasaidia makandarasi hata kupata zabuni za nje. "Waliua vyama vyote wakabaki na kimoja na sasa hivi kazi zote za Benki ya Dunia wanazidaka juu kwa juu kila wakizisikia wanazikamata na bungeni wana wawakilishi watano wa kuwasemea," alisema.

Alisema ubinafsi ndio umekuwa kikwazo kikubwa cha kukwama kuanzishwa chama kimoja cha makandarasi kwani kila mtu amekuwa akijifikiria yeye binafsi badala ya jumuiya nzima ya makandarasi.

Aliwataka pia kuacha kufanyiana fitna wenyewe kwa wenyewe kwenye zabuni badala yake kila mtu aonyeshe uwezo wake kwa kufanyakazi nzuri itakayowavutia wateja wengine na serikali kwa ujumla.

Aliwataka pia makandarasi kuacha uzembe na wafanyekazi kwa uaminifu kwani ubabaishaji ndio ulisababisha serikali kuweka utaratibu wa kufanyakazi yenyewe kwa kutumia utaratibu wa force account.

Msajili Msaidizi wa Bodi hiyo, (Utafiti na Maendeleo), David Jere, alisema makandarasi 69 walishiriki mafunzo hayo.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (watano kulia), akiwa pamoja na baadhi ya wafanyakazi wa NMB, alipokuwa akizungumza wakati anashukuru kutunukiwa tuzo ya kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki wa Mwaka (Bank CEO of The Year) katika hafla ya kuwatunuku wanawake viongozi (Financial Women Awards) iliyofanyika ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waomba shule kupandishwa hadhi ya sekondari

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKAZI wa Kata ya Mundindi wilayani Ludewa wameiomba serikali kupitia Wizara ya Elimu kuipandisha hadhi Shule ya Elimu Maalum ya Mundindi kuwa ya sekondari ili kuwanusuru wanafunzi wanaofanya vizuri wasibaki nyumbani.

Ombi hilo walilitoa wakati wa makabidhiano ya bweni la kulala wanafunzi na pikipiki, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 57 kutoka Shirika la Maendeleo la Padeco.

Mmoja wa wananchi hao Mary Kilasi, alisema watoto hao wana uwezo mkubwa wa kufaulu masomo yao darasani, lakini ndoto zao zinaishia njiani kutokana na kukosa shule ya kuendelea wanapofaulu.

Naye Diwani wa Kata ya Mundindi, Wice Mgina, alisema ipo haja kwa shule hiyo kupandishwa hadhi na kuwa na kidato cha kwanza hadi cha nne ili kuwanusuru wanafunzi wanaofaulu wasikwame kuendelea na elimu ya sekondari.

"Kwa sababu tunaona kuna miaka miwili nyuma watoto wamefaulu lakini wamekosa fursa ya kwenda kusoma, unamtoa mtoto hapa unampeleka sekondari ya kata anafika kule anakutana na walimu wengine na walezi wengine hawajui kabisa namna ya kumlea," alisema Mgina.

Aliiomba serikali kuiongezea kidato cha kwanza hadi cha nne shule hiyo ili baada ya kuhitimu masomo yao waweze kuendelea na elimu ya juu katika maeneo mengine.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Amos Mtitu, alisema shule hiyo ina wanafunzi 83 na imekuwa na maendeleo mazuri ya wanafunzi kufaulu.

"Shule ina maendeleo mazuri kitaaluma kwa sababu wapo wanafunzi wanaofaulu mitihani yao ya mwisho na kujiunga na shule ya sekondari kwa mfano mwaka 2021 shule imekuwa nafasi ya pili kiwilaya katika kundi lake kwa kufaulisha kwa asilimia 100," alisema Mtitu.

Mkurugenzi wa Shirika la Padeco, Wilbard Mwinuka, alisema katika kuadhimisha miaka kumi ya shirika hilo tangu lianze shughuli za maendeleo mkoani Njombe wamekabidhi bweni la wanafunzi wa wavulana, vitanda vya juu na chini 25 pamoja na magodoro 50 ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali za kutoa elimu bora kwa Mtanzania.

"Pia hapa shuleni tumekabidhi pikipiki aina ya honda yenye thamani ya Shilingi milioni tatu pamoja na vifaa vitakavyo wawezesha watoto hao kukaa kwenye pikipiki kwa usalama zaidi kama kiti na mwamvuli ili kutumika kuwasafirisha wakati wa dharura inapojitokeza," alisema Mwinuka.

# KCU yaanza kukopesha wakulima pembejeo

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

CHAMA Kikuu cha Ushirika (KCU) 1990 LTD mkoani Kagera kimeanzisha mfuko wa kuwakopesha pembejeo wakulima wa zao la kahawa ambao ni wanachama ili walime kwa tija.

Mpango huo umebainishwa na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Respicius John, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu mpango wao wa kuwasaidia wakulima.

John alisema kwa kutambua kuwa chama kikuu kinaundwa na wakulima kupitia vyama vya ushirika, kimeamua kuwasaidia ili wasiuze zao hilo likiwa shambani.

"Tumeanzisha mfuko maalum wa kumkopesha mkulima ili kutatua matatizo na kero mbalimbali zinazolalamikiwa vipindi vilivyopita kuhusu kutopata fedha za kuendesha kilimo na kujikimu," alisema John.

Alisema mkulima akikosa fedha za kuhudumia shamba lake na kujikimu inakuwa rahisi kushawishika kuuza kahawa mbichi ikiwa shambani.

Alifafanua kwamba kupitia mpango huo, mkulima atakuwa anakopa fedha kipindi ambacho siyo cha msimu wa mavuno ya kahawa na muda wa kuvuna ukifika atalazimika kupeleka kahawa yake katika chama hicho kuuza ili alipe mkopo.

"Endapo mkulima atakopa pesa kwenye kipindi ambacho sio cha msimu wa mavuno, itasaidia kwenda kuendesha kilimo na kukidhi mahitaji, itabidi sasa akivuna alete kahawa yake ili alipe mkopo," alifafanua John.

John alisema chama hicho kinaundwa na AMCOS 134 zenye wakulima zaidi ya 50,000 ambao wanalima zao la kahawa kila mwaka.

"Na sisi chama kikuu tunahakikisha kile kinachopatikana kinarudishwa kwa wakulima kama sehemu ya kuwahamasisha wazalishe kwa wingi," alisema. Aliongeza kuwa ili kuendelea kuwasaidia wakulima hao, wamepanga kuanzisha vitega uchumi viwe dhamana ya benki wanapohitaji mikopo.

Alisema kwa kutambua kuwa zao la kahawa ni kilimo biashara kwa Mkoa wa Kagera, kikiwekewa mifumo mizuri kinaweza kutoa ajira kwa vijana wengi.

# Wazazi na walezi wasisitizwa kuwajibika malezi ya watoto

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imetoa wito kwa wazazi, walezi pamoja na jamii kutekeleza wajibu wao wa malezi pamoja na makuzi kwa watoto wao walioko masomoni, na si shule ama walimu pekee kuachiwa jukumu hilo.

Aidha, imesema kutokana na kukua kwa utandawazi na mazingira duni kwenye jamii wanamoishi wanafunzi, kumechangia vijana walio katika kundi la kupevuka kuharibika kimaadili. Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam, akizindua bweni la wasichana katika Shule ya Sekondari Loyola, lililojengwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Marekani kupitia mpango wa shule, hospitali nchi za nje (USAID-ASHA) kwa Sh. bilioni 1.8.

Alisema ukosefu wa shule zenye bweni humwongezea vikwazo mtoto wa kike na kuongeza mdondoko wa wasichana masomoni, kutokana na mazingira magumu ya kufuata shule lipo huku usafiri kuwa wa tabu hususan maeneo ya miji mikubwa.

"Uwiano kati wavulana na wasichana kwenye shule za sekondari hauendani. Takwimu za mwaka 2021 zinaonyesha uwiano wa wanafunzi wa kidato cha tano na sita upo chini, kwani katika kila wavulana 10 masomoni wasichana ni saba pekee," alisema Prof. Mdoe.

Pia Prof. Mdoe aliema uwiano wa wavulana na wasichana upande wa shule za msingi una matumaini na kwamba hata wanafunzi walioko kidato cha kwanza hadi nne shule za sekondari takwimu zinaridhisha huku takwimu za mwaka 2021 zikibainisha kuna kuliko na wavulana 10, wasichana ni 11, walioko masomoni.

Alibainisha kwamba nchi kwa kushirikiana na wadau ikiwamo shule binafsi inahitaji kuimarisha ushirikiano, akisema takwimu za mwaka 2021, zinaonyesha kati shule za msingi 18,546 zilizopo nchini, 1,890 zinamilikiwa na mashirika na watu binafsi na kati ya shule za sekondari 5,289 zilizo chini ya watu binafsi ni 1,287.

Akisoma risala kwa niaba ya wanafunzi, Priscila Kihyoza alisema siku njema zinakuja miongoni mwa wanafunzi wasichana baada ya mazingira ya masomo kuendelea kuboreshwa, akisema vikwazo walivyokumbana navyo ikiwamo usafiri, vilirudisha juhudi masomoni.

Awali Mkuu wa Shule hiyo, Padri Martin Waweru, alisema sababu ya shule hiyo kuanzisha bweni ni kuondokana na changamoto za malezi na makuzi ya wanafunzi ikiwamo ugumu wa usafiri, mazingira ya mtaani na ushirikiano duni kwa baadhi ya wazazi na walezi na kwamba bweni litakuwa na uwezo wa kuhudumia wasichana 453.

Aidha, Padri Waweru aliiomba serikali kuboresha mfumo wa ushindani akisema hautoi uwiano sawa hasa kwa shule za bweni, wanafunzi wengi na kwamba kuwepo bei elekezi ya vitabu na vifaa vya kitaaluma.

Mkurugenzi wa Mkazi wa USAID, Kate Somvongsiri, alisema kwamba uandikishaji wa wavulana na wasichana kwenye shule za msingi ni karibu sawa, ingawa viwango vya kumaliza sekondari kwa wasichana vinarudi nyuma.

"Ndoa za utotoni na mimba na kutothamini mafanikio ya wasichana ni vikwazo. Ujenzi wa mabweni haya utaongeza uandikishwaji na wasichana waishio katika mazingira magumu kubaki shule na kupunguza athari wanazokabiliana nazo kila siku kwenda na kurudi shuleni," alisema Kate.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kheri James, alisema kwamba iwatambue na kuwathamini wadau wanaochangie elimu, akisema mchango huo hudumu kwa kizazi na vizazi, kuliko michango mingine ambayo jamii huipa kipaumbele ikiwamo harusi na sherehe zingine za muda mfupi.

Nipashe Spotika



XI WALIOONYESHA KIWANGO BORA ZAIDI EPL MSIMU HUU UK. 12



# NIGERIA VS GHANA QATAR 2022

## ●●●Ushindani wa pilau bora ulivyohamia kwenye soka

**ABUJA, Nigeria**

UKITAJA mchezo kati ya Nigeria dhidi ya Ghana, kwa wengi yatakuja mambo mawili makubwa - ushindani wa hali ya juu kwenye soka na chakula kinachoitwa 'Jollof rice', (pilau) ambacho ni maarufu Afrika.

Kwa kifupi ni pilau la asili ama wali unaochanganwa na viungo mbalimbali ikiwamo nyanya, vitunguu na pilipili ikipikwa pamoja na samaki ama nyama.

Wakati mjadala ukiendelea na kitendawili cha taifa gani ni bora kwenye kuandaa pilau nzuri kati ya mataifa hayo mawili kikiwa bado hakijateguliwa, hoja ya taifa gani kati ya hayo ni mbabe katika soka pengine inaweza kuamulia kwa sasa kupitia mchezo wa kesho, Jumanne, Machi 29.

Mataifa hayo mawili yalikutana mjini Kumasi nchini Ghana Ijumaa ya Machi 25 kwenye mchezo wa kwanza wa mchujo wa kuwania nafasi ya kufuzu Fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar baadaye mwaka huu, ikiwa ni tukio linaloadhimisha miaka 50 ya ushindani mkali wa soka kwa nchi hizo za Afrika Magharibi.

Mchezo huo ulimalizika kwa sare ya bila kufungana na kesho ndio marudiano na utapigwa jijini Abuja nchini Nigeria na mshindi atafuzu kwenda Qatar.

Timu hizo zimekutana kwa mara ya kwanza katika miaka 11 na kwa mara ya kwanza katika mechi ya kufuzu kuelekea Kombe la Dunia tangu 2001.

Super Eagles wanajiandaa kufuzu Kombe la Dunia kwa mara ya nne mfululizo, na mara ya sita kwa ujumla, wakati Ghana ambayo imefuzu mara tatu, wanataka kurejea katika fainali hizo baada ya kushindwa kufuzu fainali za mwaka 2018 nchini Urusi.

**NDUGU WAKUBWA, MAFANIKIO KIDOGO**

Kuna mechi chache sana ambazo zina athari za kitamaduni na kihisia ambazo zinaweza kuieleza mechi hii kati ya Nigeria na Ghana.

Mataifa hayo mawili yalisimama bega kwa bega tena mstari wa mbele katika vita vya kupigania uhuru kutoka kwa utawala wa kikoloni katika miaka ya 1950, wakati Ghana ilikuwa na jamii kubwa ya wahamiaji wa kutoka nchini Nigeria hadi miaka ya 1980.

Kwa kigezo cha idadi kubwa ya watu iliyonayo, Nigeria - yenye idadi kubwa zaidi ya watu barani Afrika ya karibu milioni 200 - ni wazi kwamba ni nchi kubwa kuliko mpinzani wake.

Nigeria ilifungwa bao 1-0 na Tunisia katika mchezo wa mwisho wa Kombe la Mataifa ya Afrika 2021 nchini Cameroon.

Hata hivyo, kwa upande wa soka, Ghana imeipiku Nigeria kwa mafanikio: Ikitwaa Kombe la Mataifa ya Afrika mara nne, Nigeria mara tatu, ikicheza robo fainali ya Kombe la Dunia (licha ya kushiriki mara chache ukilinganisha na Nigeria na imeshinda michezo 21 dhidi ya 10 mataifa hayo yalipokutana katika mashindano mbalimbali.

Hata hivyo, Ghana imeshinda zaidi katika kipindi cha miaka ya 1970 na 1980 ambapo Ghana ilikuwa inatawala soka la Afrika, lakini tangu ushindi wa 2-1 wa Black Stars mwaka 1992 dhidi ya Super Eagles katika nusu fainali ya Kombe la Mataifa, mambo yalianza kubadilika.

Tangu wakati huo, Nigeria ikapanda na kupata mafanikio katika soka la Afrika kati ya mwaka 1994 na 2013, na kuongeza taji lao la mwaka 1980 wakati Ghana - mabingwa mara nne wa Afrika - hawajashinda taji hilo tangu mwaka 1982, badala yake wamekuwa wakikaribia tu kufikia mafanikio ya kutwaa mataji katika kipindi cha miongo minne iliyopita.

Kabla ya mechi hiyo ya mchujo, Ghana ilichelewesha kutangazwa hadharani kwa kikosi chao hadi kufikia mwishoni mwa mwezi, ikitajwa kuwa "mkakati" uliobuniwa ili kuhujumu maandalizi ya kambi ya Nigeria.

"Na wamechanganyikiwa sana," Mjumbe wa Baraza Kuu la Shirikisho la Soka la Ghana (GFA), Sammy Anim Addo, aliieleza BBC kabla ya kutangazwa kwa kikosi hicho.

"Hatuwezi kufanya kitu kile kile kila wakati na kwa mara ya kwanza huu ni mkakati na tunaamini. Tutaifunga Nigeria na kufuzu Qatar 2022."

Chini ya benchi jipya la ufundi, Otto Addo kama kocha na mchezaji wa zamani wa Tottenham, Chris Hughton akiwa mkurugenzi wa kiufundi, Ghana iliingia uwanjani mbele ya mashabiki wake wa Kumasi bila nahodha wake aliyesimamishwa kwa kadi, Andre Ayew.

Nigeria pia iliwakosa uwanjani nyota wake kadhaa, Alex Iwobi na kiungo wa kati wa Leicester City, Wilfred Ndidi (majeruhi).

Tangu kupangwa kwa droo ya michezo hii ya kufuzu kombe la dunia, kutoka ukanda wa Afrika, mashabiki wa Nigeria wameonekana kuwa na hamasa zaidi.

**WAPINZANI WA KIHISTORIA**

Ushindani kati ya Ghana na Nigeria umekuwapo kwa muda mrefu.

Ghana ilikuwa taifa la kwanza la Waafrika weusi kupata uhuru wake kutoka kwenye utawala wa kikoloni mwaka 1957 na Nigeria ilipata uhuru wake mwaka 1960. Wanigeria wengi wakihisi kwa sababu taifa lao ni kubwa lilipaswa kupata uhuru wake kabla ya Ghana.

Ushindani ama uhasama kwenye soka ulianza tangu wakati huo nchi hizo zikipigania uhuru, huku Ghana ikishinda mechi za kwanza kwanza za kirafiki katika miaka ya 1950, ikiwa ni pamoja na ushindi wa 7-0 Juni 1955 dhidi ya Nigeria ambayo wakati huo ilikuwa ikiitwa 'Red Devils' (Mashetani Wekundu).

Mvutano wa kisiasa ulianza baina ya mataifa hayo ya Afrika Magharibi baada ya agizo la Serikali ya Ghana la mwaka 1969, kuamuru wageni wote wasio na vibali vya kuishi Ghana kuondoka.

Ingawa kulikuwa na raia wengi kutoka Togo, Burkina Faso, Ivory Coast, Niger na mataifa mengine ya Magharibi waliokuwa wanaishi nchini humo, lakini idadi kuwa ya raia wa kigeni waliokuwa wanaishi Ghana wakati huo walikuwa ni Wanigeria - hasa wa kabila la Yoruba.

Baadhi yao walikuwa nchini humo kwa miaka mingi na walikuwa katika vizazi vyao vya pili na vya tatu, hivyo tangazo hilo halikuwapendeza Wanigeria - walihisi kana kwamba zoezi hilo ama tangazo hilo liliwalenga wao.


Mambo yalibadilika wakati mafuta yalipogundulika Nigeria na uchumi wa Ghana uliporomoka, ikimaanisha kuwa kuanzia mwaka 1974, kukawa na msururu wa raia wa Ghana waliokimbilia kwenda Nigeria kutafuta ajira.

Karibu muongo mmoja baadaye, biashara ya uchimbaji mafuta ulishuka kwa sababu ya soko la dunia na uchumi wa Nigeria ulishuka, hilo likasababisha serikali kuagiza zaidi ya wahamiaji milioni moja wa Afrika Magharibi, wengi wao wakiwa ni raia wa Ghana, kuondoka Nigeria haraka mwaka 1983.

Matukio hayo ya mwaka 1983 mara nyingi huongeza na hutawala mjadala wa mashabiki kutoka pande zote kabla ya nchi hizo kukutana uwanjani, na mchezo wa kesho unaweza kuwa na tofauti kubwa sana.

### ISIKUPITE

PEP Guardiola ndiye kocha mwenye asilimia kubwa ya ushindi kwenye mechi za Ligi Kuu England katika historia ya ligi hiyo. Ameiongoza timu yake mechi 219 akishinda 162 sawa na asilimia 74, anafuatiwa na Sir Alex Ferguson; mechi 810, ushindi 528 sawa na asilimia 65 wa tatu ni Jurgen Klopp; mechi 249, ushindi 159 sawa na asilimia 64.



Extra Time



# XI WALIOONYESHA KIWANGO BORA ZAIDI EPL MSIMU HUU

**LONDON, England**

MSIMU wa Ligi Kuu England, EPL, 2021-22 ni mojawapo ya misimu bora zaidi katika historia ya hivi karibuni, na timu nyingi zikizidi matarajio. Jedwali la ligi ni gumu katika ncha zote mbili hivi sasa, huku kukiwa na upinzani mkali wa kushuka daraja na kuwania ubingwa.

Makala haya yanakiangalia kikosi cha wachezaji 11 'First Eleven' waliofanya vizuri zaidi kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Kikosi hiki cha wachezaji 11 kilichaguliwa baada ya kuzingatia ukadiriaji wa ubora wa mchezaji husika kwenye nafasi yake.

**Kipa: Jose Sa (6.96)**

Ilipotangazwa kuwa Rui Patricio angeondoka Wolves baada ya kocha, Nuno Esprito Santo, kulikuwa na hali ya kutokuwa na uhakika miongoni mwa mashabiki. Je, mbadala wake ataweza kuiga ubora wake na kiwango cha uchezaji alichofanya katika muda wake klabuni? Jose Sa bila shaka ameondoa hofu hiyo kutokana na uchezaji wake msimu huu.

Sa yuko katikati mwa timu ya Wolves ambayo imekuwa moja ya timu ngumu zaidi kufungika kwenye Ligi Kuu. Kipa huyo wa Ureno alitua hapo kutoka Olympiakos na ameruhusu mabao 23 pekee katika mechi 27 za ligi msimu huu. Amecheza mechi tisa bila kuruhusu bao huku akikabiliwa na mikwaju 111 msimu huu na kuokoa hatari 94 (sawa na asilimia 83.8%). Sa ameisaidia sana Wolves msimu huu, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, haonyeshi dalili za kupunguza kasi yake.

**Beki wa Kulia: Trent Alexander-Arnold (7.59)**

Akiwa katika kila msimu tangu awe mchezaji wa kawaida katika Klabu ya Liverpool, Trent Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 23, amekuwa mchezaji muhimu kwa timu ya kocha Jurgen Klopp katika msimu huu pia. Beki huyo wa kulia amekuwa bora zaidi katika nafasi yake kutokana na uchezaji wake akiwa na 'Wekundu' hao, ambao wanawania taji la Ligi Kuu na Manchester City.

Alexander-Arnold pia ana uwezo wa kushambuliaji na kusababisha matatizo kwa timu yoyote, na ametengeneza mabao 11 msimu huu, mawili yakiwa chini ya rekodi yake binafsi ya mabao 13.

**Beki wa Kati: Virgil Van Dijk (7.22)**

Kama ilivyokuwa kawaida kwa miaka michache iliyopita, Virgil Van Dijk bado ni mmoja wa wachezaji bora zaidi kwenye Ligi Kuu England na kwa Liverpool. Beki huyo wa Uholanzi amerejea katika kiwango bora msimu huu baada ya jeraha la bahati mbaya alilopata msimu uliopita.

Van Dijk ana mafanikio ya asilimia 88.9 ya kukaba msimu huu na amefunga mabao matatu kwa 'Wekundu' hao. Beki huyo pia ameokoa hatari 110 msimu huu kwa upande wake.

**Beki wa Kati: Joel Matip (7.29)**

Wakati Liverpool ilipotangaza kumsajili Ibrahima Konate majira ya joto, ilitarajiwa kuwa chipukizi huyo wa Ufaransa angeshirikiana na Van Dijk. Joel Matip, hata hivyo, hajaruhusu hili kutokea kwa sababu ya ubora wake.

Matip amecheza mechi 21 za ligi akiwa na 'Wekundu' hao na ana bao moja kwa jina lake. Raia huyo wa Cameroon na Ujerumani, ameokoa hatari 80 na kushinda mara 22 kati ya 29 alizojaribu kushambulia. Amekuwa kiungo muhimu sana wa timu msimu huu kwa Liverpool.

**Beki wa Kushoto: Joao Cancelo (7.45)**

Kumnunua beki wa pembeni wa Ureno, Joao Cancelo ni mojawapo ya biashara bora ambayo Manchester City imefanya katika miaka ya hivi karibuni. Alisajiliwa kutoka Juventus kwa makubaliano ya kubadilishana na Danilo, na amevutia sana wakati wake pale Etihad.

Cancelo amecheza zaidi kama beki wa kushoto wa timu hiyo na amefanya vema kwa upande wake msimu huu. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno ana bao moja na asisti tano katika mechi 26 alizocheza msimu huu kwenye ligi. Ameisaidia timu yake kubaki dhabiti na kuonyesha kiwango chake katika nafasi ya beki wa kushoto msimu huu.

**Kiungo wa Ulinzi: Rodri (7.34)**

Kiungo wa kati wa Hispania, Rodri ndiye mrithi kamili wa nahodha Fernandinho pale Manchester City. Mchezaji huyo wa zamani wa Atletico Madrid amekuwa na ujuzi wa kucheza kwenye safu ya kiungo kwa upande wake na ni mtaji mkubwa kuwa naye.

Rodri ana mabao matatu na asisti moja kwa jina lake msimu huu. Pia ametengeneza nafasi 57 kwa Manchester City kutokana na nafasi yake. Mhispania huyo amekuwa tegemeo la kweli kwa Man City msimu huu.

De Bruyne

Kiungo wa Kati: Kevin De Bruyne (7.45)

Kevin De Bruyne ameonekana kurejea katika kiwango bora zaidi akiwa na Manchester City msimu huu, huku akipania kuwaongoza kutwaa taji lingine la Ligi Kuu. Kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji ana mabao tisa na asisti tatu kwa Man City katika mechi 21 za ligi msimu huu. Kiungo huyo pia ametengeneza nafasi 84 kwa kikosi hicho kwenye ligi msimu huu.

**Kiungo wa Kati: Conor Gallagher (7.28)**

Chipukizi wa England, Conor Gallagher yuko katika msimu wake wa pili tu kwenye Ligi Kuu England, lakini amevutia macho ya kila mtu kwa uthabiti wake. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, pia ameitwa kwa mara ya kwanza katika timu ya taifa na akacheza mechi yake ya kimataifa kutokana na uchezaji wake mzuri akiwa na Crystal Palace.

Gallagher amekuwa mmoja wa viungo bora wa safu ya kati wa ligi msimu huu. Amefunga mabao nane na kutoa pasi tatu za mabao katika mechi 24 alizoichezea Palace msimu huu.

**Winga wa Kulia: Mohamed Salah (7.78)**

Mchezaji wa Liverpool, Mohamed Salah, ana msimu wa maisha yake kwa 'Wekundu' hao kwenye Ligi Kuu. Mshambuliaji huyo wa Misri amekuwa msukumo mkubwa mno kwa Liverpool huku wakilenga kuiondoa Manchester City kwenye mbio za ubingwa wa ligi.

Salah amefunga mabao 19 na asisti 10 kwa Liverpool msimu huu na ndiye kinara wa ligi. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, pia alikuwa Mwafrika aliyefunga mabao mengi zaidi katika historia ya ligi hiyo msimu huu.

**Winga wa Kushoto: Sadio Mane (7.37)**

Nyota wa Senegal na Liverpool, Sadio Mane, kama Salah, amekuwa mmoja wa wachezaji waliowaongoza 'Wekundu' hao msimu huu. Binafsi, Mane amekuwa na msimu mzuri kwa Liverpool pamoja na kushinda AFCON akiwa na Senegal.

Mane ana mabao 12 na kusaidia Liverpool kwenye ligi msimu huu. Winga huyo pia amekuwa na mchango mkubwa kwa kikosi chake huku wakifukuzia ubingwa wa Ligi Kuu.

**Mshambuliaji: Heung-Min Son (7.31)**

Mchezaji nyota wa Korea Kusini, Heung-Min Son amekuwa mmojawapo wa taa chache zinazomulika vizuri katika msimu ambao umekuwa wa kukatisha tamaa kwa Tottenham Hotspur. Mshambuliaji huyo amefanya vema kwa Spurs chini ya kila kocha msimu huu.

Son ana mabao 11 na asisti tano katika mechi 23 alizoichezea Tottenham msimu huu. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Korea Kusini ameanzisha ushirikiano mkubwa na Harry Kane, na wanashikilia rekodi ya kuwa wachezaji wawili wa kuunganishwa kwa mabao katika historia ya Ligi Kuu England.

## Nukuu


"Nina hofu hii kuhusu kustaafu, nini kitatokea baadaye? Najua nitakuwa na uwezekano na ofa nyingine, lakini raha hii ninayohisi nikiwa uwanjani, najua sitaipata popote pengine. Ndiyo maana ninakuwa na hofu hii. Nitaendeleza kadri niwezavyo na kuifurahia tu. Tutaona muda ukifika naweza kupumzika au kutoweka kabisa," **Mshambuliaji wa AC Milan na Sweden, Zlatan Ibrahimovic**



"Tunapaswa kuwa waaminifu. Kamwe hatutakubali chochote kabla mambo hayajaamuliwa; daima tutajitutumua na kujitutumua hadi kikomo. Hatuwezi kufanya lolote lingine. Hatutakubali chochote kabla mambo hayajaamuliwa," **Kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel akikataa kuiweka kando timu yake katika nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England**



"Nina uhakika [Jürgen] Klopp anafanya yote anayoweza kufanya ili klabu isimame kidogo. Kupata mbadala wa Mohamed Salah ni jambo lisilowezekana kabisa. Je, hiyo itagharimu kiasi gani? Liverpool wamepata chaguzi zingine za ubora katika safu ya ushambuliaji, lakini Salah ndiye anayehusika kwa mabao mengi. Kama ataondoka kutakuwa na jukumu kubwa kwa wachezaji wengine. Ingeacha pengo kubwa kama angeondoka," **Mchambuzi wa soka England, Paul Robinson**



# WACHEZAJI 8 KUTOKA NJE WALIVYOIPAMBA STARS



Mchezaji wa Taifa Stars Novatus Dismas (jezi namba 24), akishangilia baada ya kuifungia Stars bao dhidi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati, akiwa na Adi Yusuph (jezi namba 22) pamoja na wachezaji wengine. **MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza kwenye historia ya soka Tanzania, Taifa Stars imekuwa na wachezaji wanane wanaocheza soka nje ya nchi.

Wachezaji hao wameitwa kwenye kikosi cha timu ya taifa na wote walicheza kwenye mechi ya kirafiki iliyo kwenye Kalenda ya Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), Jumatano iliyopita ilipoitandika Afrika ya Kati mabao 3-1, Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Baadhi walionekana kwa mara ya kwanza kuichezea Timu ya Taifa ya Tanzania, huku wengine wakiwa ni wale waliozoeleka. Wachezaji wote hao waliotoka nje walicheza, sita walianza, wawili wakiingia kipindi cha pili.

Huenda kesho tena wakaonekana wakati timu hiyo itakapocheza tena mechi yake ya pili ya kirafiki ya kimataifa iliyo kwenye Kalenda ya FIFA dhidi ya Sudan.

Huko nyuma, timu ya taifa ya Tanzania haijawahi kuita idadi kubwa kama hii ya wachezaji, wanaosakata kabumbu la kulipwa nje ya nchi kwenye michuano yoyote ile, iwe mechi za kirafiki, Kombe la Chalenji, kufuzu AFCON, au Kombe la Dunia.

Hawa ndiyo wachezaji wanane walioing'arisha Stars ambao waliletwa kutoka nje ya nchi...

**#1. Haji Mnoga - Weymouth**

Alishawahi kuichezea timu ya Taifa ya England chini ya miaka 17 mwaka 2019. Kwenye mechi ya Jumatano iliyopita dhidi ya Afrika ya Kati, alicheza kama beki wa kulia. Alizaliwa Portsmouth nchini England, timu yake mama ni Portsmouth, lakini anaichezea timu ya madaraja ya nchini, Weymouth kwa mkopo. Haji ana umri wa miaka 19 na kwenye timu ya taifa, Taifa Stars alivaa jezi namba 28. Ameitwa kwa mara ya kwanza kwenye kikosi hicho.

**#2. Novatus Dismas - Beitar Tel Aviv Bat Yam**

Alicheza kama kiungo mkabaji kwenye mechi dhidi ya Afrika ya Kati na kuvaa jezi namba 24. Si mara ya kwanza kuichezea Stars, na anajulikana na mashabiki wengi wa soka nchini, kwani alishazichezea timu za Azam FC, ambayo nayo ilimpeleka kwa mkopo Biashara United hadi ilipomuuza nchini Israel kwa klabu maarufu ya Maccabi Tel Aviv mwaka 2020. Kwa sasa anaichezea klabu ya Beitar Tel Aviv Bat Yam, akiwa na miaka 19, na ndiye aliyefunga bao la kwanza Jumatano iliyopita dhidi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati.

**#3. Ben Starkie - Spalding United**

Mashabiki wa soka Tanzania pia walimwona mchezaji mwingine akiichezea kwa mara ya kwanza Taifa Stars. Huyu ni Ben Starkie ambaye alivaa jezi namba 23. Jina lake kamili ni Ben Antony Swakali akiwa na umri wa miaka 19 kwa sasa.

Huyu pia alizaliwa England, huko Leicester, lakini tofauti yake na Mnoga ambaye aliichezea timu ya Taifa ya England chini ya miaka 17, huku alishaichezea timu ya Tanzania chini ya miaka 20 mwaka jana. Kwenye mechi dhidi ya Afrika ya Kati, alicheza kama kiungo mshambuliaji. Kwa sasa anaichezea Klabu ya Spalding United, ambao inacheza Ligi ya Kanda, Kaskazini mwa England.

**#4. Kelvin John - KRC Genk**

Alicheza kama namba tisa kwenye mechi hiyo, ikiwa ni heshima kubwa kwake kupishwa na nahodha wa timu hiyo Mbwana Samatta. Kelvin John ambaye anadai Samatta ndiye aliyemfanya kupambana kucheza soka ili aonekena na yeye aende nje ya nchi, amepata bahati ya kwenda kwenye klabu hiyo ambaye mwenzake ametoka ya KRC Genk. Haitaji maelezo mengi kwani mashabiki wengi wanamfahamu licha ya umri wake mdogo. Hajazunguka sana, ingawa amecheza timu karibuni za umri wote za vijana, kwa sasa yupo kwenye Klabu ya KRC Genk ya Ubelgiji. Jezi yake ni namba tisa.

**#5. Abdillahie Yusuph - Yeovil Town**

Si mara ya kwanza kwa straika huyu kuicheza Taifa Stars, kwani aliwahi kuitwa mara kadhaa. Naye alianza kwenye kikosi cha Jumatano iliyopita dhidi ya Afrika ya Kati, akivaa jenzi namba 22, akicheza nafasi ya namba 10.

Adi Yusuph kama anavyoitwa, ni mzaliwa na Zanzibar, miaka 30 iliyopita, lakini kwa sasa anaichezea klabu ya Yeovil Town ya nchini England, ambayo kwa mfumo wa soka la nchini humo, ipo daraja la nne.

**#6. Mbwana Samatta - Antwerp**

Ndiye nahodha ya Taifa Stars. Hahitaji maelezo mengi, mbali ya kumtaja kuwa ni mchezaji wa zamani wa Simba, TP Mazembe, KRC Genk, Aston Villa na Fenerbahce ya Uturuki ambayo ni klabu yake mama, lakini kwa sasa anaichezea Antwerp ya Ubelgiji kwa mkopo, akifunga bao la pili kwenye mechi dhidi ya Afrika ya Kati.

**#7. Simon Msuva - Wydad Casablanca**

Pamoja na kwamba ana mgogoro na klabu yake, kiasi cha kumfanya arejee nchini na kutocheza kwa muda sasa, lakini haiondoi ukweli kuwa ni mchezaji wa Klabu ya Wydad Casablanca ya Morocco hadi hapo kesi itakapoisha au FIFA kuamua vinginevyo. Na ndicho kwa asilimia kubwa kimempa hata heshima ya kuitwa kwenye kikosi hicho, aliingia kipindi cha pili kwenye mechi hiyo.

**#8. Joshua Mwakasaba - Tusker**

Ukiangalia kwenye orodha ya wachezaji wote nane wa Stars, ni wawili tu wanaocheza soka la kulipwa barani Afrika nje ya Tanzania. Ni Msuva na straika huyu ambaye aliingia kipindi cha pili kwenye mechi dhidi ya Afrika ya Kati.

Ameitwa Stars kutoka kwenye Klabu ya Tusker ya Kenya. Ameweka rekodi ya kuwa mchezaji pekee wa Tanzania anayecheza soka la kulipwa ndani ya Afrika Mashariki nje ya Tanzania kuitwa. Kabla ya kujiunga na timu hiyo alikuwa kwenye klabu ya Lipuli ya Iringa.

**JE, WAJUA?**



STEVEN Pienaar ndiye mchezaji kutoka Afrika Kusini anayeshikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi zaidi za Ligi Kuu England (214), akifuatiwa na Lucas Radebe (197) na watatu ni Mark Fish (124).



# Wadau waombwa maoni kuboresha mitaala

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetoa wito kwa wadau wa elimu kutoa maoni yao ya kuboresha mitaala ya elimu kwa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia ili kuwa na elimu bora.

Mkurugenzi msaidizi wa mafunzo kwa walimu wa wizara hiyo, Huruma Mageni, alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu wanaofundisha somo la hisabati.

Mageni alisema kwa sasa serikali inapitia mitaala ya elimu nchini kuanzia ngazi ya awali hadi vyuo ili kuboresha masuala mbalimbali ambayo yamekuwa yakitolewa kasoro na wadau wa elimu nchini.

"Hivi sasa maoni yanakusanywa na kupitiwa upya nitoe wito kwa wadau mbalimbali wa elimu kuleta maoni yao na wizara itayafanyia kazi ili kupata kitu kilicho bora kwa masalahi mapana ya taifa letu,"alisema Mageni.

Akizungumzia kuhusu mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu walipo kazini kufundisha somo la Hisabati, alisema yatatatua kero zilizokuwepo kwenye ufundishaji wa somo hilo.

Alisema hivi sasa kuna tatizo katika ufundishaji wa somo hilo nchini, hali ambayo inachangia wanafunzi wengi kufanya vibaya katika matokeo yao ya mwisho.

"Kumekuwa na changamoto kubwa ya ufundishaji wa somo la hisabati nchini hata ukiona katika matokeo mbalimbali mitihani ya somo la hisabati imekuwa chini sana katika ufaulu ufundishaji wa hisabati unategemea sana mbinu za walimu na ufundishaji wa somo lenyewe," alisisitiza.

Kiongozi wa mradi wa kuwajengea uwezo wa mbinu za kufundisha somo la hisabati (SITMS), Dk. Catherine Fulgence, kutoka Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam (DUSE), alisema mradi huo ni wa miezi 30.

"Mradi huu ni wa miezi 30 yaani miaka miwili na nusu na unafanyika katika nchi tatu na mimi ndiye kiongozi wake katika nchi zote na unafadhiriwa na nchi ya Canada ambapo lengo lake ni kujengea uwezo walimu wanaofundisha somo la hisabati ili kuwa na mbinu bora za ufundishaji na kuongeza ufaulu,"alisema Dk. Fulgence.

Aidha, alisema mradi huo wanautekeleza kwa kushirikia na vyuo vya ualimu pamoja na shule mbalimbali katika nchi zote tatu.

"Mradi huu upo katika nchi za Kenya, Zambia na Tanzania na kila nchi tunafanya na vyuo saba na kila chuo kinakuwa na shule tano ambazo zipo jirani yake," alisema.

Kwa upande wake, Mbunge wa Urambo, Magreth Sitta, aliiomba serikali kuwekeza fedha katika mafunzo kwa walimu ili kuwajengea uwezo walimu wa somo hilo.

"Mafunzo kama haya ni muhimu sana. lakini wafadhili wanakuwa na fedha ambazo zinakwenda katika maeneo fulani tu, hivyo basi serikali inapaswa kutenga fedha ili kuwezesha mafunzo haya kwenda katika maeneo mengi ya nchi," alisema.

## ASA kusaidiwa ulipaji madeni ya uzalishaji mbegu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeahidi kushirikiana na Wakala wa Mbegu (ASA) kulipa madeni ya wazalishaji mbegu wenye mikataba na wakala huo, huku ikiwataka kutumia fursa hiyo kupanua mashamba na kuongeza mitaji.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao Wizara ya Kilimo, Nyasebwa Chimagu, ndiye aliyetoa ahadi hiyo alipokuwa akifungua mkutano baina ya ASA na wazalishaji mbegu jijini hapa.

Alisema wizara inafanya kazi kwa ukaribu na taasisi hiyo hivyo itashirikiana nao kuhakikisha inalipa kiasi kidogo cha fedha ambazo wazalishaji hao wanadai ili kuwapa hamasa ya kuendelea kuzalisha mbegu.

Chimagu, alisema fursa ya uzalishaji mbegu ilioko hivi sasa ni kubwa kuliko na uhitaji wa mbegu bora kwa wakulima nchini.

"Wazalishaji mbegu mnaodai msiwe na wasiwasi wowote kwa sababu serikali imejipanga kushirikiana na ASA kuhakikisha inalipa madeni yenu," alisema Chimagu.

Alisema mkataba ambao ASA umeingia na wazalishaji ni biashara, hivyo wahakikishe wanatengeneza mpango kazi ulio bora ili wazalishaji waendelee kuzalisha mbegu zilizobora ambazo zitaleta tija kwa wakulima.

Mkurugenzi huyo alisema wizara inajipanga kuanza kutembelea maeneo ya wakulima wanayozalisha mbegu, ili kubaini kero walizonazo na kuzitafutia ufumbuzi ili kuzalisha mbegu kwa ufanisi.

"Wizara tunaomba mtoe ushirikiano pale tutakapokuja kuwatembelea, ikiwamo kuonyesha ardhi ambayo mnajua zao gani linastawi ili uweke utaratibu wa kuzalisha zao hilo katika eneo husika," alisema Chimagu.

Aliwataka wazalishaji kutumia elimu walioipata katika mkutano huo kwenda kufanya mabadiliko katika kilimo cha uzalishaji mbegu wanachofanya ikiwamo kutafuta ardhi inayofaa kwa ajili ya kulima.

Naye Mtendaji Mkuu wa ASA, Dk. Sophia Kashenga, aliishukuru serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha mbegu bora zinapatikana ili kuwasaidia kuongeza uzalishaji wa mbegu bora na kukidhi mahitaji ya nchi.

Mzalishaji mbegu ambaye ni Mkurugenzi wa Aria Plantation LTD kutoka Kilosa, Msraman Modhwadin, alisema wanakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo miundombinu hali inayochangia kurudisha nyuma uzalishaji wanaoufanya.




Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, akizungumza wakati wa kufungua semina ya siku moja kwa walimu na walezi wa klabu za kupinga rushwa jijini Dodoma iliyofanyika mwisho wa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mtaka: Wanafunzi wajengewe uzalendo kupambana na rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewataka walimu walezi wa klabu za kupinga rushwa mkoani humo kuwajenga wanafunzi uadilifu na uzalendo wa mapambano dhidi ya rushwa wakiwa shuleni.

Mtaka alitoa ushauri huo alipokuwa akifungua semina ya walimu walezi wa klabu za kupinga rushwa kwenye shule za msingi na sekondari jijini Dodoma iliyoandaliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma. Mtaka alisema walimu hao wanapaswa kusaidia taasisi hiyo kufanikisha elimu ya kuzuia rushwa inawafikia wanafunzi kwa ufasaha.

"Nawapongeza TAKUKURU Dodoma kwa kuanzisha klabu za wapinga rushwa katika shule za msingi na sekondari, ombi langu kwenu walimu walezi wa klabu, simamieni kwa weledi misingi inayotakiwa katika kuelimisha wanafunzi juu ya suala la rushwa," alisema Mtaka.

Aliitaka taasisi hiyo kuweka mikakati ya kuandaa kongamano kubwa la klabu za wapinga rushwa, ambalo litawakutanisha wadau mbalimbali ambao watajadili namna ya kupambana na rushwa.

Alisema kongamano hilo litajadili masuala ya rushwa, litasaidia kupanua wigo wa wanachama wa klabu na kubadilishana mawazo ya namna ya utoaji elimu kwa jamii juu ya masuala ya rushwa. Kwa upande wake, Mkuu wa TAKUKURU mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema kuanzishwa kwa klabu hizo kumesaidia kutoa mwanga kwa jamii kujua madhara yatokanayo na upokeaji rushwa na utoaji rushwa.

Alisema uwapo wa semina hiyo kwa walimu walezi wa klabu za wapinga rushwa zinawasaidia kubadilishana mawazo na kupeana mikakati ya namna ya kupiga vita rushwa katika maeneo ya kazi.

"Klabu hizo ni muhimu sana kuwapo katika shule kwa sababu zinasaidia jamii kutoa taarifa kwa taasisi pale wanapoona miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali inakwenda kinyume," alisema Kibwengo.

Aliwataka wanafunzi walioko kwenye klabu hizo kuwa mabalozi wazuri ambao watasaidia kujenga kizazi chenye uzalendo ambacho kitasaidia kuhamasisha suala la upigaji vita.



# DC aagiza viongozi wa jiji kupanda miti kulinda chanzo maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, amewaagiza viongozi wa Kata ya Mwakibete katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya kushirikiana na wananchi kupanda miti kwenye chanzo cha maji cha Mto Nzovwe II ili kukilinda.

Dk. Chuachua alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa anazindua kampeni ya upandaji wa miti katika kata hiyo ambapo aliwataka kwenda kuchukua miti iliyooteshwa katika Ofisi za Wakala wa Usimamizi wa Misitu nchini (TFS) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema chanzo cha maji cha Mto Nzovwe ni miongoni mwa vyanzo muhimu vya maji vinavyosaidia wananchi wa Jiji la Mbeya kupata huduma ya maji ya kutosha.

Alisema maeneo yote yanayozunguka chanzo hicho yanatakiwa kupandwa miti ambayo ni rafiki kwenye vyanzo vya maji huku akiwataka maofisa wa TFS kuwaongoza wananchi hao.

"Mwanzo niliagiza kwamba wananchi wakachukuwe miti kwenye ofisi za TFS (Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania), lakini sasa nimebadili utaratibu, TFS watawaletea miti hapa ili mshirikiane kuipanda chini ya maelekezo yao," alisema Dk. Chuachua.

Alisema maeneo mengi ya chanzo hicho yako wazi hali ambayo inasababisha baadhi ya wananchi kuyafanya kuwa maeneo ya kuchungua mifugo hali inayochangia uchafuzi wa maji yanayotumiwa na wananchi.

Diwani wa Kata ya Mwakibete, Lucas Mwampiki, aliahidi kushirikiana na wananchi wake pamoja na maofisa wa TFS kupanda miti hiyo kwa maelezo kuwa wao ni miongoni mwa wanufaika wa chanzo hicho na hivyo wana wajibu wa kukilinda.

Alisema mara nyingi wananchi wamekuwa wakiharibu vyanzo vya maji kwa sababu ya kukosa elimu sahihi ya vyanzo vya maji na hivyo akawaomba maofisa wa TFS na taasisi zingine zinazosimamia mazingira kutoa elimu kwa wananchi.

Meneja wa TFS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Cosmas Ndakidemi, alisema taasisi yake imeandaa miche ya kutosha na inagawa bure kwa wananchi wanaotaka kupanda kwa ajili ya kulinda mazingira.

Aliwataka wakazi wa Kata ya Mwakibete pamoja na maeneo mengine yanayozunguka vyanzo vya maji kwenda kuchukua miti hiyo na kuipanda kwenye vyanzo hivyo.

# Bunge lanusa 'upigaji' Hospitali ya Mbarali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), imeikalia kooni Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali baada ya kubaini harufu ya ufisadi kwenye mradi wa ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo.

Kamati hiyo imemwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum kwenye mradi huo, huku ikiagiza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuwachukulia hatua za kiutumishi watumishi watakaobainika kushiriki ubadhirifu huo.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Bonface Butondo, alitoa maagizo hayo juzi wakati kamati hiyo ilipokuwa inatoa majumuisho ya ziara yake ya siku saba katika Mkoa wa Mbeya ambako ilipiga kambi kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema kamati hiyo ilibaini kuwa hospitali hiyo imejengwa kwa kutumia fedha nyingi na muda mrefu, lakini mpaka sasa bado haijakamilika, huku baadhi ya vifaa vya ujenzi ikiwamo saruji ikiharibika bila kutumika.

Alisema kwenye ukaguzi huo maalum, CAG atatakiwa kuangalia uhalisia wa gharama zilizotumika, ubora wa kazi na muda uliotumika kutekeleza pamoja na uwajibikaji wa watendaji wa halmashauri hiyo kwenye mradi huo.

Butondo alisema kwenye ukaguzi wa mradi huo walibaini pia kwamba baadhi ya kuta zimepinda, baadhi ya majengo hayajakamilika likiwamo jengo la kuhifadhia dawa hali ambayo inasababisha dawa nyingi kuharibika na kuteketezwa.

"Tunaagiza CAG awe huru wakati wa kufanya ukaguzi huo maalum na watakaobainika kufanya uzembe, Ofisi ya Rais TAMISEMI iwachukulie hatua za kiutumishi," alisema Butondo na kuongeza:

"Lakini tunaagiza Ofisi ya Rais TAMISEMI kufanya tathmini ya vibali vinavyoombwa na halmashauri hii kwa ajili ya kuteketeza dawa maana tumebaini ni dawa nyingi zinaharibika, mwaka huu pekee dawa za zaidi ya Sh. milioni 40 wanataka kuziteketeza."

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema licha ya ofisi yake kupokea maagizo ya kamati hiyo, lakini ilishaanza kushughulikia jambo hilo ili kuhakikisha ukweli unabainika.

Alisema moja kati ya hatua ambazo wameanza kuchukua ni kumtaka aliyekuwa mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Kivuma Msangi kurejea mkoani humo kujibu tuhuma zinazomkabili kwa maelezo kuwa yeye ndiye aliyesimamia mradi huo kwa muda mrefu.

Aliomba Ofisi ya Rais TAMISEMI kuwasaidia kumrejesha Msangi mkoani Mbeya kutoka Wilaya ya Serengeti mkoani Mara ambako anafanya kazi kwa sasa akisema kuwa zipo tuhuma zingine zinazomkabili zikiwamo za kwenye ukusanyaji wa mapato.

"Lakini kwa sasa ili kutokuharibu mwenendo wa ukaguzi namwagiza Katibu Tawala, watumishi wote waliokuwa wanasimamia mradi ule warejeshwe ofisini kwangu, watakaa pale muda wote na wasipangiwe kazi yoyote na hata huyo msangi atakaa pale," alisema Homera.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Switbert Mukama, alisema ukaguzi unaofanyika kwa sasa ni shirikishi, hivyo akawataka watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kutoa ushirikiano kwa CAG.

Aliipongeza kamati hiyo kwa kazi nzuri ya ukaguzi wa miradi katika mkoa huo, na kwamba kuwa ukaguzi huo unaisaidia wizara kujua hali ya utekelezaji wa miradi nchini.

Miaka ya hivi karibuni baada ya serikali kutoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kukamilisha mradi huo, ilibainika kuwa nyaraka za utekelezaji wa awali zilikuwa hazijulikani zilipo, hivyo kuibua maswali mengi.



Wajasiriamali wa Kimasai wakiwa wamepumzika kwenye kivuli huku wametundika bidhaa zao kwenye mti katika Uwanja wa Shule ya Msingi Makongorosi wilayani Chunya, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Watiwa mbaroni kwa tuhuma za wizi

**Na Nebart Msokwa**, MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia watu wawili kwa tuhuma mbalimbali za wizi akiwamo mwanamke mmoja ambaye anadaiwa kuwa kinara wa kuvunja nyumba na kuiba.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Ulrich Matei, alimtaja mwanamke huyo kuwa ni Lucy Mwalongo (20), mkazi wa Kijiji cha Ubaruku wilayani Mbarali.

Alisema mwanamke huyo alikamatwa hivi karibuni nyumbani kwake katika Kata ya Ubaruku wilayani Mbarali kufuatia msako maalumu uliofanywa na makachero wa jeshi hilo, baada ya kupata taarifa za siri kuhusu mwanamke huyo kujihusisha na wizi majumbani.

Kamanda Matei alisema baada ya kumpekua nyumbani kwake, mwanamke huyo alikamatwa na mali mbalimbali za wizi zikiwamo nguo, vyombo vya muziki pamoja na vitu vingine vingi ambavyo vyote aliiba sehemu moja.

Alisema kwenye ukaguzi huo mbali na nguo pamoja na vyombo pia alikutwa na simu za mkononi, kadi za benki za watu mbalimbali pamoja na redio moja.

"Mali zote zlizokutwa nazo mwanamke huyo zina thamani ya Sh. 900,000 na zote zilitambuliwa kuwa aliziiba nyumbani kwa Raphael Edward (34), mkazi wa Ubaruku wilayani Mbarali na tunaendelea na upelelezi wa shauri hili," alisema Kamanda Matei.

Katika tukio lingine, Kamanda Matei alisema jeshi hilo linamshikilia kijana mmoja aitwaye Geofrey Maliatabu (18) mkazi wa Ubaruku wilayani Mbarali kwa tuhuma za kukutwa na pikipiki ya wizi. Kamanda Matei alisema kijana huyo alikamatwa akiwa anaitumia pikipiki hiyo aina ya Kinglion yenye Chasisi namba LZLP 900 KHH50839 akiwa amenyofoa namba za usajili ili isifahamike.

Kamanda Matei alisema walipompekuwa kijana huyo walibaini kuwa alikuwa hana nyaraka zozote zinazoonyesha kuwa pikipiki hiyo ni mali yake na ndipo wakaamua kumsweka ndani na kuwataka watu wote waliopotelewa na pikipiki kwenda kuitambua pikipiki hiyo.

Alisema jeshi hilo linaendelea na upelelezi ili kubaini mtandao mzima wa wizi wa pikipiki katika mkoa huo ili kuudhibiti mapema huku akiwataka wananchi waendelee kushirikiana na jeshi hilo kwa kutoa taarifa za matukio ya wizi.

Alisema kutokana na ushirikiano ulioko kati ya wananchi na Jeshi la Polisi kwa sasa mkoa huo umefanikiwa kupunguza matukio ya uhalifu, huku akieleza kuwa wezi ni miongoni mwa makundi yaliyodhibitiwa vizuri zaidi.

Alisema katika siku za hivi karibuni, jeshi hilo limewanasa wezi mbalimbali akiwamo mtu mmoja aliyetoroka na fedha za bosi wake Sh. milioni 26 ambazo alitumwa kuipeleka benki.





Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Makame, akipata maelezo kuhusu ufugaji wa chatu kwa mtembeza watalii, Idrisa Muhammed, katika ushirika wa wananchi wenye mashamba eneo la Jozani Mkoa wa Kusini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Rais Mwinyi ampongeza Blair kuendelea kuiunga mkono Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameampongeza Waziri Mkuu mstaafu wa Uingereza, Tony Blair, kwa kutekeleza kwa vitendo ahadi zake za kuendelea kuiunga mkono Zanzibar hasa katika mipango na mikakati ya upangaji wa vipaumbele kwa watendaji wa serikali.

Rais Dk. Mwinyi alitoa pongezi hizo alipofanya mazungumzo na Waziri Mkuu mstaafu huyo Ikulu Zanzibar ambaye yupo kwa ziara maalum.

Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa kupitia Taasisi ya Tony Blair Institute for Global Change, imeweza kuunga mkono jitihada za serikali ya kutoa mafunzo kwa watendaji wakuu juu ya upangaji wa vipaumbele, hatua ambayo ina umuhimu mkubwa katika mipango ya serikali.

Alisema mafunzo hayo ambayo taasisi hiyo iliyatoa kwa watendaji wa Serikali ya Zanzibar yana mchango mkubwa katika mipango ya serikali na utekelezaji wake.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi alimhakikishia kiongozi huyo kwamba serikali itaendelea kuthamini michango ya Taasisi ya Tony Blair Institute for Global Change, kwa sababu imeonyesha nia na dhamira kubwa ya kuiunga mkono Zanzibar ili mipango yake ya maendeleo kufanikiwa ipasavyo.

Naye Blair alimweleza Rais Dk. Mwinyi hatua zinazoendelea kuchukuliwa na taasisi yake katika kuhakikisha malengo na mikakati ya kuiunga mkono Zanzibar yanatekelezeka na kuzaa matunda. Alisema taasisi yake imeshaweka mipango kabambe katika kuhakikisha inatoa mchango mkubwa katika kuhakikisha mipango iliyopangwa na serikali anayoiongoza Rais Dk. Mwinyi inatekelezeka.

Taasisi hiyo imeshatoa mafunzo ya upangaji wa vipaumbele kwa watendaji wakuu wa serikali ya wakiwamo makatibu wakuu, wakurugenzi, maofisa wadhamini na watendaji wengine, yaliyofanyika Februari mjini Zanzibar.

# Eneo la kuanika dagaa kuwa la uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, amesema eneo la kuanika dagaa lilioko Fungu Refu Mkoa wa Kaskazini Unguja linahitaji kuimarishwa ili kuwa eneo muhimu la uwekezaji.

Alitoa kauli hiyo wakati wa ziara zake katika mkoa huo na kutembelea eneo la wajasiriamali waanika dagaa katika Kijiji cha Fungurefu.

Alisema kwa vile eneo hilo lina shughuli nyingi na limetoa ajira kwa watu tofauti, linapaswa kuwa kituo kikubwa cha waanika dagaa katika mwambao wa Afrika Mashariki na Kati.

Alisema serikali kupitia miradi yake itajenga gati ya kuegeshea vyombo vya uvuvi, soko la samaki na kuimarisha huduma muhimu ikiwamo miundombinu ya maji na umeme na huduma zingine za kibinadamu ili kuwe na mazingira salama kwa watumiaji wa eneo hilo.

Eneo la Fungurefu ni maarufu kwa shughuli za uanikaji dagaa likiwa na watu zaidi ya 8,000 na boti za uvuvi zaidi ya 1,000.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Aboud Suleiman Jumbe, alisema katika eneo hilo kuna changamoto nyingi ikiwamo miundombinu ya barabara.

Alisema katika kuzitafutia changamoto zilizoko katika eneo hilo, wameshakaa na taasisi husika zikiwamo Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFIKO) na Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo na vya Kati (SMIDA) ili kuwa na mipango madhubuti ya kutatua changamoto hizo.

Katika hatua nyingine, waziri huyo alitembelea Kisiwa cha Mnemba katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na kusema kuwa serikali itachukua hatua za makusudi ili kukinusuru kisiwa hicho kisiendelee kuchukuliwa na bahari na kiendelee kuleta haiba kwa watalii.

Alisema kisiwa hicho kina historia ndefu na ni miongoni mwa visiwa vyenye uwekezaji kwa muda mrefu na kinachangia mapato ya serikali, hivyo kinapaswa kuwekewa mikakati imara ili kisizidi kuathirika na mabadiliko ya tabianchi.

Jonathan Braack, Meneja wa mradi katika Kisiwa hicho, alisema hadi sasa zaidi ya mita 40 kutoka usawa wa bahari zimeshaliwa na kusababisha baadhi ya miti kung'oka na athari za kimazingira zinaongezeka, hali inayoashiria kutoweka kwa kisiwa hicho muhimu miongoni mwa visiwa vya Zanzibar.

# Waandishi wahimizwa kuhubiri amani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC), Abdallah Abdurahman Mfaume, amewataka waandishi wa habari kuendelea kuwa mabalozi wazuri katika kuhubiri amani ya nchi.

Akizungumza jana na Nipashe Mjini Zanzibar kuhusu ujenzi wa amani, alisema waandishi wa habari wana dhamana kubwa kuendelea kudumisha amani ili Zanzibar iendelee kustawi kiuchumi.

Alisema amani inapochafuka nchini maendeleo hayataweza kupatikana, hivyo ni vyema kuwa mabalozi wazuri kwa jamii kuendelea kuhubiri amani na kujikita katika kusuluhisha migogoro.

"Migogoro inapotokea katika jamii waandishi wa habari tusiwe sehemu ya kuchochea migogoro bali tuwe wasuluhishi wazuri wa kutatua migogoro hiyo bila ya kumwonea mtu," alisema.

Asia Bakari, mmoja wa wanufaika wa mafunzo ya utatuzi wa migogoro, alisema baadhi ya nchi zimetumbukia katika migogoro na umwagaji damu usiokwisha kutokana na kuichezea amani.

Alisema migogoro katika jamii haiepukiki, lakini ni vyema ikasuluhishwa kabla haijasababisha madhara.

"Ili jamii ipate maendeleo lazima kuwe na utofauti wa mawazo, lakini hii isiwe sababu ya kugombana na hatimaye kuhasimiana kwa sababu sote ni wamoja na tunajenga nyumba moja," alisema.

Aidha, alizishauri taasisi zinazojitolea kuhamasisha amani na utatuzi wa migogoro kuendelea ili kuhakikisha Zanzibar na Tanzania zinaendelea kuwa visiwa vya amani.

Katibu Mkuu wa ZPC, Mwinyimvua Abdi Nzukwi, aliipongeza Taasisi ya Search for Common Ground (SCG) na Umoja wa Ulaya (EU) kwa kuziunga mkono taasisi za kizalendo kutoa elimu kuhusu utatuzi wa migogoro.

Alieleza kuwa, ZPC ni miongoni mwa wanufaika wa mradi wa utatuzi wa migogoro unaotekelezwa kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya.

"Tumewajengea uwezo waandishi wa habari kuwa sehemu ya watatuzi wa migogoro kwa kutumia kalamu zao kwa sababu wao wanaifikia jamii kubwa," alisema.

# TOSCI yamaliza tatizo mbegu feki

**Na Mwandishi Wetu, MOROGORO**

TAASISI ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), iliyo chini ya Wizara ya Kilimo, imemaliza tatizo la mbegu feki na dhaifu zilizokuwa zikiuzwa kwa wakulima wa nchini na kuwasababishia hasara baada ya taasisi hiyo kuongeza kasi ya matumizi ya nembo zenye ubora katika mbegu zinanazozalishwa.

Akizungumza na gazeti hili mjini hapo, Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Patrick Ngwediagi, alisema katika kipindi cha mwaka 2014/2015 matukio ya mbegu feki na dhaifu yalikuwa kati ya 300 mpaka 350 hali iliyoleta hasara kwa wakulima nchini.

Alisema baada ya kuwapo kwa malalamiko mengi ya wakulima kuhusu matukio ya kuuziwa mbegu hizo zisizo na tija, TOSCI iliamua kuweka mikakati mbalimbali ikiwamo kuongeza kasi ya ukaguzi na kuweka nembo zenye ubora wa kisasa.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2016/17 waliongeza kasi ya utoaji wa nembo za kisasa baada ya kufanya ukaguzi wa mbegu kutoka milioni mbili hadi milioni 10 katika kipindi cha mwaka 2019/20 na kumaliza tatizo hilo kwa kiwango kikubwa.

Alisema kutokana na udhibiti wa mbegu feki uliotokana ongezeko la matumizi ya alama, wamelisaidia taifa kuhakikisha mbegu zinazozalishwa na kupelekwa kwa wakulima zinakuwa na ubora unaotakiwa.

Pia alisema kutokana na mafanikio hayo TOSCI imeongeza uzalishaji mbegu kutoka asilimia 34 ya mwaka 2015 hadi 81 hivi sasa ya mazao yote yanayozalishwa nchini na kuwapo kwa uhakika wa mbegu bora.

Alitaja mafanikio mengine ni TOSCI kuiwezesha Tanzania kujiunga na skimu za mbegu za Shirika la Kimataifa la OECD ambalo linatambua ubora wa mbegu kutoka hapa nchini zenye nembo ya TOSCI hatua ambayo kuuza mbegu nje inayozalishwa nchini itakuwa sio tatizo.

"Tanzania kupitia TOSCI hivi sasa tumeweza kujiunga na Skimu za mbegu za Shirika la Kimataifa la OECD ambalo linatambua ubora wa mbegu kutoka hapa nchini na kupata Hati ya Ithibati ya ISTA sio nchi zote inaweza kuzipata bali ni mpaka ufikie viwango vya kimataifa," alisema Ngwediagi.

Mmoja wa wakulima wakubwa wa mazao ya nafaka katika Mkoa wa Morogoro, Thadei Hafigwa, alipongeza TOSCI kwa kupunguza tatizo la mbegu feki kwa kuwa katika kipindi cha nyuma wakulima wengi walikuwa wakipata hasara kutokana na kutokuwapo kwa udhibiti wa kampuni ya kuzalisha mbegu.

Kaimu Mkurugenzi wa uendelezaji wa mazao kutoka Wizara ya Kilimo, alisema mkakati wa sasa wa serikali ni kuachana kabisa na uagizaji wa mbegu kutoka nchi jirani na badala yake kuwatumia watalaam wa ndani kuzalisha za kujitosheleza na ziada kuuza nje ya nchi.

## Waziri Jafo awahimiza wanafunzi kupandamiti

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Seleman Jafo, amewataka wanafunzi kuanzia shule ya msingi hadi vyuo kuona umuhimu wa kupanda miti ili kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi inayolikabili taifa na dunia kwa ujumla.

Alitoa wito huo jijini Dar es Salaam wakati alipojumuika na viongozi na wadau mbalimbali wa mazingira kusafisha fukwe wilayani Kingamboni.

Alisema lengo la kampeni ya 'Soma na Mti' aliyoizindua ni kuhakikisha miti zaidi ya milioni mbili inapandwa ndani ya mwaka mmoja.

Pia Waziri Jafo alisema kuna wanafunzi zaidi ya milioni 14 katika shule za msingi, sekondari na vyuo, ambao wakishiriki kikamilifu katika upandaji wa miti itasaidia kwa kiasi kikubwa kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

"Kwa sasa kila halmashauri imeelekezwa kupanda miti milioni moja na nusu, pia niwahimize wananchi katika maeneo mbalimbali yakiwamo ya biashara na huduma za kijamii kuhakikisha wanashiriki katika zoezi la usafi wa mazingira.

"Sambamba na hilo serikali inahimiza maeneo yote wanayokaa watu zikiwamo stendi za mabasi, daladala, masoko, maeneo ya biashara mbalimbali, taasisi za serikali zote yawe katika hali ya usafi," alisisitiza.

Aliupongeza uongozi wa Wilaya ya Kigamboni na mkoa kwa ujumla kwa kutekeleza maelekezo ya serikali ya kuweka maeneo yote katika hali ya usafi jambo linalosaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza magonjwa ya mlipuko.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Fatma Nyangasa, alisema kampeni ya kuiweka wilaya hiyo katika hali ya usafi sambamba na kupanda miti inaendelea pamoja na udhibiti wa utupaji taka ovyo, huku akisisitiza kuwa kila mmoja anawajibika kwa nafasi yake kuhakikisha suala hilo linafanikiwa.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam, Hassan Rugwa, alimpongeza Waziri Jafo na wadau wengine wa mazingira kwa kujitoa katika kuhakikisha mazingira katika maeneo mbalimbali nchi yanawekwa katika hali ya usafi na kutunzwa.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu (kushoto) na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wawekezaji wa Utalii Zanzibar (ZATI), Rahim Bhaloo (kulia), wakitia saini hati za makubaliano ya kiutendaji kati ya taasisi hizo mbili mjini Zanzibar mwishoni mwa wiki. Wanaoshuhudia ni Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Mohamed (katikati), Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban (wapili kulia), Katibu Mkuu Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Fatma Mabrouk (watatu kulia) na wawakilishi wengine kutoka sehemu zote mbili. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# ZATI, Exim kukuza utalii wa Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya Wawekezaji wa Utalii Zanzibar (ZATI) na Benki ya Exim Tanzania zimetiliana saini Mkataba wa Makubaliano (MoU) ya ushirikiano wa kiutendaji hatua inayolenga kuinua kuboresha utoaji kwa sekta ya utalii katika visiwa hivyo ya kihistoria.

Ushirikiano huo unatoa wasaa kwa wadau hao wawili kushirikiana katika kuhakikisha taarifa zote muhimu kuhusu utalii visiwani humo Zanzibar zinapatikana kwa urahisi duniani kote na kuhakikisha kwamba wanachama wa ZATI wanapata ufumbuzi wa mahitaji yao yote ya huduma za kifedha.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya utiaji saini makubaliano hayo iliyofanyika Zanzibar mwishoni mwa wiki, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Mohamed pamoja na kuwapongeza wadau hao wawili kwa hatua hiyo, alitayataja makubaliano hayo kuwa ni ya aina ya kipekee yakiwa yameainisha viashiria mahususi vya utendaji kwa pande zote mbili ili kuwezesha maendeleo ya miundombinu bora ya utalii na shughuli kote Visiwani.

Alisema hatua hiyo inakwenda sambamba na azma ya serikali ya kuimarisha ushirikiano miongoni mwa taasisi za sekta binafsi pamoja uhusiano baina ya serikali na sekta binafsi.

"Ni imani yangu kuwa uhusiano mzuri baina ya wadau wa serikali na taasisi za kifedha ikiwamo Benki ya Exim yatasaidia zaidi wadau mbalimbali wa utalii Zanzibar ambao wameathiriwa kwa kiasi kikubwa na athari za kiuchumi za COVID-19 ili waweze kujikwamua na hatimaye kurejesha uwezo wao wa kiuchumi," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu, alisisitiza kuwa hatua hiyo ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo kuendelea kukuza sekta ya Utalii Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

"Sekta hii muhimu ya utalii ni moja ya sehemu ambayo tunaitazama zaidi hususani katika visiwa hivi vya Zanzibar na maeneo mengine hapa nchini hivyo na niahidi kwamba tutaendelea kujizatiti zaidi hilo. Utalii ni nguzo muhimu ya uchumi wa Zanzibar na sisi tutaendelea kuzingatia hilo kwa kuwekeza zaidi muda wetu, juhudi, rasilimali watu na mtaji zaidi katika kuhudumia sekta hii na msimamo wetu huo hautabadilika" alisisitiza.

Kwa mujibu wa makubaliano hayo ya miaka mitatu, benki hiyo itahusika katika kuhakikisha wadau wa utalii wanapata mikopo ya biashara kubwa na ndogo inayoandaliwa kulingana na mtiririko wa fedha za mwanachama husika.

"Pia tutaendelea kutoa huduma bora zaidi za kubadilishia fedha kwa kuzingatia viwango vyenye ushindani zaidi kwa sarafu zote ikiwamo Shilingi ya Kitanzania pamoja na Dola ya Kimarekani. Pia tunahakikisha wanapata huduma nyingine nyingi ikiwamo huduma za bima, uwepo wa makubaliano maalum katika viwango vya ushuru pamoja na kuwapatia mashine za malipo (POS)," alisema Matundu.

Mwenyekiti wa ZATI, Rahim Bhaloo, alipongeza Benki ya Exim kwa ushirikiano huo, na kusema hatua hiyo itaiwezesha sekta ya kimkakati ya utalii Zanzibar kuongeza kwa kiasi kikubwa uwezo wake, kuinua ubora wa huduma na kuongeza zaidi mvuto wa Visiwa hivyo kwa watalii wa ndani na nje ya nchi.

"Ni muhimu kueleza kuwa hatua hii ni matokeo ya ushirikiano wa karibu na wenye tija kati ya ZATI na wadau wake wakiwemo wanachama wake, taasisi za fedha kama Benki ya Exim na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ushirikiano huu huu utatuwezesha kusaidia ipasavyo biashara yetu ya utalii, kutengeneza ajira, na kuboresha ustawi wa wawekezaji wadogo na wakubwa katika sekta ya utalii," alisema.

## '50/50 jitihada zinahitajika kumnyanyua mwanamke'

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema ili kufikia usawa 50/50 katika maendeleo, juhudi kubwa zinahitajika kumnyanyua mwanamke kwa kuwa anapitia changamoto nyingi zinazomrudisha nyuma.

Waziri Gwajima aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam, katika warsha ya 'Kungwi na Mwali' ikiwa ni kampeni ya kuhamasisha wanawake kupambana na kansa ya kizazi iliyoandaliwa na kampuni ya Brembo.

Alisema wanawake wapo mstari wa mbele katika, masuala ya kimaendeleo, lakini wana majukumu makubwa ya kijamii tofauti na wanaume ikiwamo kulea watoto, wazee na wagonjwa, kupika na kuchota maji.

"Kitaifa asilimia 80 ya nguvu kazi katika sekta ya kilimo ni wanawake ambao uzalishaji wake ni asilimia 60, hivyo wana nafasi kubwa katika taifa hili, wanahitaji kuwezesehwa kiuchumi na kuelimishwa kujua nafasi yao katika jamii ili wajiamini na kusonga mbele katika ujenzi wa taifa," alisema.

Vile vile, alisema katika kuhakikisha mwanamke anawezeshwa, mwaka jana, Rais Samia Suluhu Hassan alizindua kamati ya kitaifa itakayokuwa inatoa ushauri wa jinsi ya kumwezesha wanamke kiuchumi na sasa ipo katika hatua ya kuandika mapendekezo ya nini kifanyike ili kufanikisha azma hiyo.

Waziri Gwajima aliishukuru kampuni hiyo kwa kuanzisha kampeni inayolenga maendeleo ya wanawake na jamii kwa kuwa inamtambua rasmi kama mdau wa masuala hayo kwa kuwa serikali inatafuta watu wa namna yake wa kushirikiana nao.

"Serikali imekuwa ikisema kuwa tuna upungufu wa rasilimali watu, kumbe tunao wadau walioko katika sekta binafsi ambao wakiwezeshwa wanaweza wakafika kule ambapo serikali imeshindwa," alisema Waziri Doroth.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Brembo, Naswiyat Brembo, alisema kampeni ya Kungwi na Mwari, inafanyika kila mwaka ikihusisha masuala ya kiuchumi, afya na malezi ya jamii ambayo yana mchango mkubwa katika kutekeleza maazimio mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

"Mwaka huu tumejikita kumwelimisha mwanamke juu ya afya ya kizazi, na hii imetokana na kampuni yetu kuguswa na madhara yanaowakumba kwa kuingiza dawa za kienyeji katika sehemu zao za siri, na kuleta athari ikiwamo kansa ya kizazi, hali inayowarudisha nyuma kimaendeleo," alisema Naswiyat.

"Unakuta mtu anauza dawa za kienyeji zenye mchanganyiko wa viungo vya kupikia kama vitunguu saumu, binzari, mdalasini na kuwaambia wanawake kuwa wakipaka sehemu zao za siri basi zitakuwa kama vile hawajazaa, kitu ambacho ni hatari kwa kuwa hakijathibitishwa na wataalamu wa tiba," alisema.

Alisema aliamua kuhamasisha kuhusu suala hilo kwa sababu ameshafuatwa na wanawake wenye matatizo ya maambukizi katika njia ya haja ndogo (UTI) sugu na alipowauliza wengi wao walikiri kutumia vitu kama hivyo.

# Kampuni ya Puma kuuza gesi ya nyumbani

**Na Mary Geofrey**

KATIKA kudhibiti uharibifu wa mazingira nchini, kampuni ya mafuta ya Puma Energy, imejitosa kwenye biashara ya kuuza nishati ya gesi ya nyumbani nchini.

Mwenyekiti wa Bodi ya kampuni hiyo, Dk. Seleman Majige, alisema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, wakati akitoa tuzo kwa wasambazaji na watoa huduma ya mafuta kwenye vituo vya mafuta nchini.

"Suala la mazingira Watanzania wengi wanatumia kuni hivyo katika kukabiliana na tatizo hili, tumeona nasi tuongeze nguvu katika mapambano haya ya kutunza mazingira kwa kuanza kuuza nishati ya gesi," alisema Dk. Majige.

Alisema wanatarajia kuanza kutoa huduma hiyo mwezi Mei mwaka huu, katika vituo vyao vyote vya mafuta nchini.

Dk. Majige alisema kampuni hiyo inaendelea kuhakikisha mafuta yanakuwa salama na kuitaka menejimenti kuweka mkakati wa kuanzisha vituo vijijini ili huduma hiyo iwafikie wananchi wengi zaidi.

Aliwakumbusha watoa huduma kutumia maneno mazuri kwa wateja kwa sababu ni silaha ya kufikia mafanikio ya kibiashara.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Dominic Dhanah, alisema kampuni hiyo ndiyo inayoongoza nchini na inashika namba moja kwa ubora.

"Kampuni imeendelea kuwa bunifu na tumeongeza huduma nyingine ya vilainishi vya kwenye magari na mapema mwaka huu, tunatarajia kuzindua nishati ya gesi ya nyumbani ambayo itakuwa inapatikana kwenye vituo vyetu vyote na hakuna shaka kwamba itapokelewa vizuri," alisema Dhanah.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (kulia), akizungumza katika hafla ya utoaji tuzo za shindano la Malkia wa Nguvu 2022 jijini Dar es Salaam juzi. Tuzo hizo ziliandaliwa na Clouds Media Group (CMG). Katikati ni Mkurugenzi wa Biashara na Uwekezaji wa CMG, Shebs Kusaga na Mkurugenzi Mtendaji, Joseph Kusaga. **PICHA: SABATO KASIKA**

## UVIKO-19 ilivyoathiri mapato ya utalii Burunge WMA

**Na Salome Kitomari, aliyekuwa BABATI**

MAPATO ya utalii katika Hifadhi ya Jamii ya Burunge, Wildlife Management Area (WMA), yameporomoka kutoka Sh. bilioni mbili hadi Sh. milioni 400 kwa mwaka, hali inayosababisha baadhi ya miradi ya huduma za kijamii kusuasua kutokana na ugonjwa wa UVIKO-19.

Hayo yalibainika mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), waliotembelea WMA kujionea shughuli za uhifadhi, utalii na kijamii pamoja na mapito ya wanyamapori ya Kwakuchinja, chini ya mradi wa Tuhifadhi Maliasili wa Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID).

Katibu wa Burunge WMA, Benson Mwaise, alisema tangu kuanza kwa ugonjwa wa UVIKO-19 mwaka 2020 mapato yalipungua kwa vijiji vilivyokuwa vinapata mgawo wa Sh. milioni 104 vikapata milioni 68 na sasa yameendelea kushuka zaidi.

"UVIKO-19 ni changamoto kubwa sana, mapato yalishuka chini ya mara tatu, miradi ya kijamii kwenye baadhi ya vijiji ilisimama kwa ukosefu wa fedha na wengine kuanza kuchangishana jambo ambalo tulishalisahau kwa zaidi ya miaka 10," alisema na kuongeza:

"Tumevishauri vijiji 10 vinavyounda Burunge WMA kwa kipindi hiki kuwa na miradi rahisi isiyohitaji fedha nyingi, tumeona baadhi ya maeneo wameanza kukimbia makazi yao kwasababu ya michango ya huduma za kijamii."

Mwaise alisema kwa sasa wageni wengi wanaowapokea ni wa ndani na WMA ilifika wakati ilishindwa kulipa mishahara ya watumishi na kuwapunguza ili iweze kuendelea kujiendesha.

Alisema mapato ya WMA iliyoanzishwa mwaka 2006 yenye ukubwa wa kilomita za mraba 283 ikiwa ni eneo lililotolewa na vijiji vya Mwada, Sangaiwe, Ngolley, Vilima Vitatu, Kakoi, Minjingu, Olasiti, Maweni, Magara na Manyara yalianza kwa Sh. milioni 300.

Alisema yaliendelea kuongezeka hadi mwaka 2019/20 walipata zaidi ya Shilingi bilioni mbili na kila kijiji kilipata mgawo wa Sh. milioni 104, na kwamba fedha hizo hugawanywa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) asilimia 25 na Halmashauri ya Babati Vijijini asilimia 10 inayobaki ni ya WMA.

Alisema kutokana na hali hiyo wanafanya jitihada za kuelimisha wananchi kuendelea kuhifadhi maliasili hiyo ikiwamo ubunifu, ili waendelee kuona faida ya maeneo waliyotenga kisheria kwa ajili ya kuunda WMA hiyo.

"Migogoro baina ya binadamu na wanyama inazidi kuongezeka, lakini bado tunaelimisha wananchi umuhimu wa uhifadhi kwa kuangalia miradi waliyotekeleza kutokana na fedha za uhifadhi, walivyosomesha watoto wao na kuboresha maisha yao, siyo rahisi, lakini wengi wanaelewa na kuendelea kutunza hii raslimali."

Baadhi ya wakazi wa kijiji cha Sangaiwe kinachopakana na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Burunge WMA, Nicodemas Mofulu, alisema wanajivunia uhifadhi kwa kuwa umewapatia fedha nyingi ikiwamo kuwa na hoteli mbili zinazomilikiwa na kijiji, na kutokana na mapato kupungua mwaka huu walipata mgawo wa Sh. milioni 48.

Alisema mapato ya hoteli zao yaliporomoka kutoka Sh. milioni 30 hadi 40 kwa mwezi na sasa wanapata chini ya milioni tatu au nne kwa kipindi hicho, lakini hawajakata tamaa kwa kuwa wanaamini UVIKO -19 ikiisha watapata fedha nyingi.

HABARI MICHEZO

# KABANGU ACHAPWA, AMSHUSHA KIDUKU AKIMTAJA MWAKINYO BORA

**Saada Akida na ShufaaLyimo**

LICHA ya Bondia Mtanzania, Twaha Kassim 'Kiduku', kushinda kwa pointi dhidi ya Alex Kabangu kutoka DR Congo, Mkongomani huyo amesema kwake Hassan Mwakinyo ndiye bondia bora zaidi kwa hapa Tanzania.

Kiduku juzi alinyakuwa ubingwa wa Afrika Universal Boxing Organization (UBO), baada ya kumpiga Kabangu kwa pointi katika pambano la raundi nane lililofanyika mjini Morogoro.

Akizungumza baada ya pambano hilo, Kabangu alisema kwa hapa Tanzania Mwakinyo ndiye bondi bora zaidi kwa upande wake na wala si mingine yeyote.

"Nasema na nitaendelea kusema kwamba Kiduku sio bondia bora hapa Tanzania, bondia ninayemkubali na bora kwa Tanzania hii ni Hassan Mwakinyo," alisema Kambagu baada ya kupigwa na Kiduku.

Kwa upande wa Kiduku, alisema anafurahi kuona amefanikiwa kuwapa raha Watanzania kwa kumchapa Kabangu katika pambano hilo la ubingwa wa Afrika.

Alisema mchezo ulikuwa mzuri na kwamba ushindi wake ulitokana na kusoma vema mbinu za mpinzani wake huyo.

"Mchezo ulikuwa mzuri, watu wengi walitarajia nitashinda kwa KO, lakini Watanzania ushindi ni ushindi na nimeweza kuitangaza vema bendera ya Tanzania na kuweka heshima kwa taifa langu," alisema Kiduku.

Wakati huo huo katika pambano hilo kulikuwa na mapambano ya utangulizi ikiwamo bondia kutoka Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), George Bonabucha, kufanikiwa kutetea ubingwa wake wa PST dhidi ya Juma Fundi.

Najma Isike aliibuka na ushindi baada ya kumtwanga Halima Bandola kwa pointi kwenye pambano la raundi sita.

Bondia Juma Misumali alishindwa kuendelea na pambano dhidi ya Joseph Kafrikoko kwenye pambano la raundi sita uzani wa (Middle Weight kg 76).

Paul Magester aliibuka na ushindi wa pointi baada ya kumchapa Shabani Kabuji kwenye pambano la raundi sita uzito wa Bantam Weight Kg. 54.

## BADO KIDOGO...



Utandikaji wa nyasi bandia kwenye Uwanja wa Kituo cha Michezo cha Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), uliyoko Kigamboni, Dar es Salaam ukiendelea kwa kasi kama unavyoonekana pichani. Uwanja huo una ukubwa wa eneo la kuchezea sawa na ule wa Benjamin Mkapa huku mwingine utakaokamilika katika awamu hii ya kwanza ukiwa ni wa nyasi asili. **PICHA: TFF**

# Arusha wang'ara tena Tanga City Marathon

**Na Cheji Bakari, Tanga**

WANARIADHA kutoka mkoani Arusha wanaume na wanawake wameng'ara katika mashindano ya Tanga City Marathon Season 6 katika umbali wa kilometa 21 na 10 hii ikiwa ni mara ya sita mfululizo kwao kufanya vizuri, tangu yalipoanzishwa mwaka 2017.

Katika mashindano hayo yaliyofanyika jana jijini hapo na kushirikisha wakimbiaji zaidi ya 1500 kutoka mikoa mbalimbali nchini Tanzania na Kenya, kwa upande wa wanaume kilometa 21, Merson Mbuya kutoka Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU), alikuwa mshindi wa kwanza baada ya kutumia muda wa saa 1:05, nafasi ya pili ilienda kwa Mathayo Sumbi kutoka Arusha aliyetumia saa 1:10, huku mshindi wa tatu akiwa ni Elisha Wema kutoka Arusha akitumia saa 1:12:01

Kwa upande wa wanawake kilometa 21 mshindi wa kwanza ni Lucia Senga kutoka Kilimanjaro akitumia saa 1:06:01 mshindi wa pili Consolata Lyimo kutoka Arusha akitumia saa 1:14:08 na mshindi wa tatu ni Eliupendo Suley kutoka Arusha ametumia saa 1:15:19.

Aidha, kwa upande wa mbio za kilometa 10 wanaume mshindi wa kwanza ni Rinta Pakua kutoka Efm Jogging Club Dar es Salaam ambaye alitumia dakika 31:00:01, mshindi wa pili alikuwa ni Kisanta Steven kutoka Dar es Salaam ambaye alitumia dakika 45:08 na watatu akiwa ni Samson Chemu wa Dar es Salaam ambaye alitumia dakika 46:02.

Kwa upande wa wanawake mshindi wa kwanza ni Prisca John kutoka Karatu aliyetumia dakika 40:15, akifuatiwa na Mwajuma Shembu akitumia dakika 45:21 na mshindi wa tatu akiwa ni Scolastica Hamisi kutoka Tanga ametumia dakika 47:32.

Mshindi wa kwanza kilometa 21 kwa wanawake na wanaume waliibuka na zawadi ya Sh. 400,000 na medali huku mshindi wa pili akitia kibindoni Sh. 300,000 na medali na wa tatu akiondoka na Sh. 200,000 na medali.

# Alliance yaipania Yanga Uhuru leo

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Alliance Girls, Sultan Juma, amesema wachezaji wake wako fiti kwa ajili ya kuwavaa wenyeji wao, Yanga Princess katika mchezo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Alliance Girls itakuwa ugenini dhidi ya Yanga Princess katika mchezo utakaopigwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Sultan alisema wamejiandaa vizuri na wachezaji wake wako fiti kuhakikisha wanarejea Mwanza na pointi muhimu katika mchezo huo.

Alisema hana mchezaji yeyote majeruhi katika kikosi chake na wote waliokuwapo katika msafara wa kwenda Dar es Salaam kwa kwa ajili ya mechi hiyo, wapo tayari kuhakikisha wanapata pointi tatu dhidi ya Yanga Princess.

"Yanga ni timu nzuri ina makocha wazuri, tutaingia uwanjani kwa kuwaheshimu na kucheza kwa tahadhari kubwa, lakini lengo letu ni kutafuta pointi tatu," alisema Sultan.

Alliance Girls ipo nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi hiyo, ikiwa na pointi 15 huku Yanga wakiwa nafasi ya nne kutokana na kujikusanyia alama 17 hadi sasa.

# Makata aipigia hesabu Biashara

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Mbeya Kwanza, Mbwana Makata, amesema amejipanga vizuri kuivaa Biashara United Aprili 6, mwaka huu, watakapoifuata mkoani Musoma kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makata alisema anachokifanya kwa sasa katika kikosi chake ni kuyaendeleza mazuri yote yaliyoacha na mtangulizi wake.

"Kwa sasa anaendeleza yale mazuri yote aliyoyaacha mwalimu aliyepita pamoja na kurekebisha makosa madogo madogo," alisema Makata.

Alisema mchezo huo dhidi ya Biashara United unatarajiwa kuwa mgumu na wenye ushindani mkali, kwani kila timu inajipanga kupata matokeo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### YOURI KWA ARSENAL, UNITED
KLABU ya Manchester United na Arsenal zote zimehusishwa kutaka kumnunua Youri Tielemans, ambaye anaweza kuruhusiwa kuondoka Leicester kwa kitita cha pauni milioni 35 mwisho wa msimu huu. ***(Metro)***

### POGBA AWINDWA PSG
PSG wamemfanya kiungo wa kati wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29, kuwa shabaha yao kuu ya uhamisho. ***(Fabrice Hawkins,via Express)***

### MOSES AZUIWA KUTUA EPL
LIGI Kuu England imezuia jaribio la Burnley kutaka kumsajili winga wa Nigeria, Victor Moses mwenye umri wa miaka 31, kutoka klabu ya Urusi ya Spartak Moscow. ***(Sky Sports)***

### TIELEMANS AITAKA UEFA
KIUNGO wa kati wa Leicester City na Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 24, amesema anataka kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Mirror)***

### WINKS KUNG'OLEWA SPURS
KLABU ya Southampton na Crystal Palace zina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa England, Harry Winks mwenye umri wa miaka 26 kutoka Tottenham. ***(Star)***

### PSG YAMTAKA LUKAKU
KLABU ya PSG ya Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, msimu ujao inaweza kumsajili mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku, 28. ***(Football Insider)***

### DYABALA KUMRITHI MARTINEZ
MSHAMBULIAJI wa Argentina, Paulo Dybala, anaweza kuhama kutoka Juventus kwenda kwa wapinzani wao wa Serie A, Inter Milan, huku wakimpanga mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kama mbadala wa Muargentina mwenzake, Lautaro Martinez, 24. ***(Mail)***

### HAALAND PASUA KICHWA
MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland atahamia Manchester City au Real Madrid msimu huu, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, amekataa ofa ya kwanza kubwa ya Manchester City. ***(AS)***

### OSIMHEN ADA KUBWA
KLABU ya Napoli wanataka euro milioni 100 kwa mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 23, ambaye amepokea ofa kutoka kwa klabu kadhaa zikiwamo Arsenal, Liverpool, Manchester United, Newcastle na Tottenham. ***(Fichajes)***

### TRAORE HAKIELEWEKI BARCA
MUSTAKABALI wa mlinzi wa Hispania, Adama Traore mwenye umri wa miaka 26, anayecheza katika Klabu ya Barcelona kwa mkopo, unategemea kama Wolves wataamua kufanya uhamisho wa Francisco Trincao aliyeichezea Barcelona kwa mkopo kuwa wa kudumu. ***(Mundo Deportivo)***

### PSG YAMFUATILIA RAPHINA
KLABU ya Paris St-Germain inafuatilia maendeleo ya winga wa Leeds United na Brazil, Raphinha, 25. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RASHFORD AINGIA ANGA WANAOSAKWA ARSENAL

Awali walihusishwa washambuliaji kadhaa akiwamo Dominic Calvert-Lewin na Alexander Isak, lakini sasa inaonekana...

**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal inaendelea kuimarika chini ya kocha Mikel Arteta, lakini mshambuliaji ndio hitaji kubwa kwa sasa kwa klabu hiyo.

Baada ya uhusiano wake na Arteta kuzorota, Pierre-Emerick Aubameyang aliondoka kwenda Barcelona wakati wa dirisha la usajili la Januari na ameonekana kuwa kwenye kiwango bora chini ya Xavi.

Ingawa Alexandre Lacazette mambo yake yamekuwa sawa na Arsenal, yeye na Eddie Nketiah mikataba yao itakamilika mwishoni mwa msimu huu, na 'Washikabunduki' hao wanatakiwa kutafuta mshambuliaji.

Arsenal wanajiandaa kumpa ofa nyota wa Manchester United, Marcus Rashford katika jaribio la kuimarisha kikosi chao, kwa mujibu wa gazeti la The Mirror.

Arsenal walihusishwa na kusajili washambuliaji kadhaa wakati wa dirisha la Januari, akiwamo Dominic Calvert-Lewin wa Everton na Alexander Isak wa Real Sociedad, lakini inaonekana Rashford kutoka pale Old Trafford ndio chaguo kubwa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ana mwaka mmoja katika mkataba wake wa sasa, lakini anaonekana kuwa si mtu muhimu chini ya kocha wa muda, Ralf Rangnick.

Rashford ameanza mara 10 pekee kwenye mechi za Ligi Kuu England msimu huu na kufunga mabao matano katika michuano yote.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
MONTENEGRO
VERSUS
GREECE
1 | 3.23
X | 3.23
2 | 2.27

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DI MARIA: NIMEFIKIA MWISHO ARGENTINA



**BUENOS AIRES, Argentina**

ANGEL Di Maria amesema "asante, asante na asante mara elfu" kwa mashabiki wa Argentina baada ya kucheza mechi ambayo inatarajiwa kuwa ndio ya mwisho kwake kwenye ardhi ya nyumbani.

Di Maria alifunga bao moja na kutengeneza jingine katika ushindi wa mabao 3-0 wa kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Venezuela kwenye Uwanja wa La Bombonera Ijumaa - mechi ya 30 mfululizo ya 'La Albiceleste' bila kufungwa.

Mchezaji mwenzake wa Paris Saint-Germain, Lionel Messi ndiye aliyefaidika na pasi ya mabao ya Di Maria, huku Argentina wakiwa tayari wana uhakika wa kwenda Qatar, alipendekeza baada ya mechi hiyo afikirie mustakabali wake wa kimataifa baada ya Kombe la Dunia.

Di Maria alikuwa na uhakika zaidi katika maoni yake baada ya mechi, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, akitafakari juu ya "usiku mzuri".

"Nitasema tu asante kwa upendo mkubwa ambao nimepata," aliandika di Maria kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Siku zote nilikuwa nikiota kila kitu nilichoishi katika usiku huu mzuri. Pengine ilikuwa mechi yangu ya mwisho na jezi ya Argentina nyumbani, na kuweza kusema kuwa ulikuwa usiku mzuri.

"Asante, asante na asante mara elfu.

"Sasa niipongeze timu nzima kwa mechi kubwa iliyochezwa, mechi nzuri kwa wote. Tunaendelea kukua na kuwa pamoja. Twende Argentina!!!"

Di Maria amecheza mechi 121 na kufunga mabao 24 tangu aicheze kwa mara ya kwanza Argentina dhidi ya Paraguay mwaka 2008.

# Laporta: Sijui chochote hatima Dembele Barca

**BARCELONA, Hispania**

JOAN Laporta hafahamu kuwa Ousmane Dembele anaweza kutaka kubakia Barcelona, lakini alifichua kuwa mazungumzo ya mkataba na Gavi na Ronald Araujo "yako sawa".

Dembele amebakiza miezi mitatu tu katika mkataba wake na Barca na hakuna dalili ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa kukubali kuongeza muda wake wa kukaa Camp Nou.

Hata hivyo, Makamu wa Rais wa 'Blaugrana' hao, Rafael Yuste wiki hii alisema "ikiwa Dembele ataendelea kujisikia vizuri, basi tunaweza kukutana na mawakala wake na anaweza kubaki".

Rais wa Barca Laporta amesema hakuna mabadiliko yoyote kuhusu mustakabali wa mshambuliaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund, huku miamba hao wa Catalunya wakijitahidi kupigania ubingwa wa LaLiga baada ya kupata ushindi wa mabao 4-0 wa Clasico dhidi ya Real Madrid.

Aliliambia gazeti la Mundo Deportivo: "Dembele ni mvulana mzuri na wa aina yake, angalau hajatuletea matatizo tangu tulipoiongoza klabu.

"Labda tunamwona Dembele bora tangu akiwa Barca, hakika ni mchezaji ambaye makocha wanamfahamu vema zaidi, kuanzia Xavi ambaye anamsimamia vizuri mchezaji huyo.

"Lakini tulimpa ofa ya kumwongeza tena mkataba ambayo uliisha Desemba 20 mwaka jana. Aliamua kutotumia fursa. Sasa Xavi amesema alikuwa akimtegemea kwa sababu ni mchezaji anayeleta mabadiliko.

"Sasa kuongezwa upya kwa Dembele? Ngoja tuone chaguo alilokuwa nalo limeisha na tayari tunapanga viwango vya mishahara ambavyo wale wote watakaosalia msimu ujao watalazimika kuvikubali. Viwango vingine vinapaswa kudumisha uendelevu na uwiano wa klabu na kikosi."

Alipoulizwa kama Barca watatoa ofa mpya kwa Dembele, Laporta alijibu: "Kwa sasa, kwa madhumuni yetu, hatuna habari kwamba anataka kuendelea.

"Sijui kama mwakilishi wake amekuwa akiwasiliana, lakini nadhani si kwa sababu angejua na kimsingi tunazingatia hatua hii ya mwisho ya ligi kujaribu kufanya makubwa na kushinda.

"Mwisho wa msimu, nadhani kwa namna fulani kutakuwa na mazungumzo lakini ndani ya viwango vya mishahara ambavyo tunaanzisha."

Kiungo chipukizi Gavi na mlinzi wa Uruguay, Araujo wana mkataba na Barca hadi mwisho mwa msimu ujao, lakini Laporta hana wasiwasi wowote kuhusu mustakabali wao.

Alisema: "Hii iko kwenye njia sahihi. Ndio, ni wachezaji ambao tunataka kuendelea nao, ndani ya viwango hivi vya mishahara tunayoanzisha. Tungependa waendelee kwa miaka mingi."

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA

# MBEYA CITY YALIA KUKAMIWA, KUBADILI MFUMO WA UCHEZAJI

**Na Dennis Fussi**



KOCHA wa Mbeya City, Mathias Lule, amesema pamoja na kuanza mzunguko wa pili vibaya kwenye Ligi Kuu, bado ana matumaini ya kufanya vizuri msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo raia wa Uganda, alisema matokeo mazuri waliyopata kwenye mzunguko wa kwanza yamesababisha timu nyingi kuwakamia.

"Mbeya City bado ni ile ile ingawa mzunguko wa pili tumeuanza vibaya kwa sababu ya timu pinzani kutukamia, hii imetufanya tushindwe kucheza mpira wetu, " alisema Lule.

Kocha huyo amesema kitu ambacho amekikusudia kukifanya ili kurudisha ushindi ni kubadili mfumo wa uchezaji tofauti na ule waliotumia mzunguko wa kwanza.

Mbeya City ipo nafasi ya tano katika msimamo wa Ligi Kuu ya soka Tanzania Bara ikiwa na pointi 25 baada ya michezo 18.

Ligi hiyo ambayo ipo mapumzikoni kupisha mechi za kimataifa zilizoko kwenye Kalenda ya Fifa, inatarajiwa kurejea Aprili Mosi, kwa Polisi Tanzania kuikaribisha Ruvu Shooting kabla ya kesho yake kupigwa mechi mbili kwa Tanzania Prisons kuialika Dodoma Jiji Mbeya City ikiwa na shughuli pevu nyumbani dhidi ya Geita Gold.

# Bahati ajivunia safu ya ushambuliaji Biashara

**Na Dennis Fussi**



KOCHA Mkuu wa Timu ya Biashara United ya Mara, Vivier Bahati, amesema anaridhishwa na ubora wa safu yake ya ushambuliaji.

Kocha huyo amesema tangu amejiunga na timu hiyo hivi karibuni, wamefunga mabao sita kitu ambacho kinampa matumaini ya kujinasua katika mstari wa kushuka daraja.

"Nina washambuliaji wenye uwezo na kipaji katika ufungaji kama Collins Opare na Chriss Zigga hawa wote wamefanya kazi yao vizuri na ndio tegemeo letu katika ufungaji," alisema Bahati.

Aliongeza kuwa, kwa sasa ana uhakika kikosi chake katika kila mchezo ulio mbele yao wataondoka na pointi zote tatu, kutokana na makali ya safu yake ya ushambuliaji.

"Kwa sasa katika kila mechi tutakazocheza nina uhakika wa kuweza kuondoka na pointi tatu, hivyo tunaendelea kujifua na kujipanga zaidi ili tuweze kujiweka kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Najua kwamba, Ligi ni ngumu, lakini na sisi tunajiona kwamba, tuna nafasi ya kufanya vizuri zaidi kwa sasa."

Biashara United ipo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Soka Tanzania Bara ikiwa na pointi 22 katika michezo 18 ilizocheza mpaka sasa

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 28/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:30 | 1949 | Neroca FC vs Pailan Arrows | 1.39 | 4.19 | 7.01 |
| 14:35 | 3945 | Aizawl FC vs Kenkre FC | 1.36 | 4.38 | 7.21 |
| 15:00 | 4302 | Anzhi Makhachkala vs Biolog Novokubansk | 2.04 | 3.01 | 3.60 |
| 17:00 | 1797 | US Biskra vs JS Kabylie | 2.67 | 2.91 | 2.62 |
| 17:00 | 2988 | Paradou AC vs MC Alger | 2.36 | 3.01 | 2.91 |
| 17:00 | 4115 | JS Saoura vs ASO Chlef | 1.44 | 3.80 | 7.01 |
| 17:00 | 4328 | FK Graficar Beograd vs FK Zlatibor | 2.25 | 2.81 | 3.34 |
| 17:00 | 5934 | FK Radnicki Sremska Mitrovica vs Backa Palanka | 2.12 | 3.00 | 3.75 |
| 17:30 | 5270 | Sreenidi Deccan FC vs Churchill Brothers | 2.41 | 3.16 | 2.72 |
| 18:35 | 1257 | AL Sahel SC vs Ohud Medina | 2.80 | 2.90 | 2.70 |
| 18:55 | 1443 | Najran SC vs AL Draih | 1.48 | 3.74 | 6.42 |
| 19:00 | 1509 | San Lorenzo de Almagro vs Rosario Central | 1.18 | 6.64 | 9.76 |
| 19:00 | 2092 | Sectzya Nes Ziona vs Hapoel Kfar Saba | 2.44 | 3.21 | 2.86 |
| 19:00 | 2382 | Hapoel Ramat Gan vs Hapoel Acre | 2.55 | 3.11 | 2.80 |
| 19:00 | 4028 | Ironi Hasharon vs Hapoel Raanana | 2.49 | 3.15 | 2.85 |
| 19:00 | 4282 | AL Khlood vs AL Jeel | 2.30 | 2.90 | 3.45 |
| 19:00 | 5935 | Jaen vs UD Almeria B | 2.90 | 3.05 | 2.50 |
| 19:30 | 1157 | Bourg Peronnas vs Laval | 2.40 | 3.07 | 2.92 |
| 20:00 | 3274 | Newcastle U23 vs West Bromwich U23 | 2.31 | 3.41 | 2.68 |
| 20:30 | 1344 | AS Tel Aviv University W vs Hapoel Marmorek Rehovot W | 1.57 | 4.08 | 4.56 |
| 21:00 | 1046 | Montenegro vs Greece | 3.23 | 3.23 | 2.27 |
| 21:00 | 1835 | CA Independiente W vs CA Platense | 1.83 | 3.74 | 3.50 |
| 21:00 | 4998 | Brown Adrogue vs Club Almagro | 2.21 | 2.97 | 3.21 |
| 21:05 | 3594 | Tristan Suarez vs Quilmes | 2.96 | 2.91 | 2.39 |
| 21:30 | 5421 | Excursionistas W vs Atletico Lanus | 3.75 | 4.18 | 1.68 |
| 21:45 | 1299 | Glentoran Belfast vs Carrick Rangers | 1.31 | 4.78 | 7.99 |
| 22:00 | 2972 | Las Palmas UD vs Leganes | 2.16 | 3.12 | 3.37 |
| 22:00 | 3147 | Orsomarso vs Real Cartagena | 2.77 | 3.06 | 2.43 |
| 22:00 | 5697 | Estudiantes BA vs Temperley | 2.13 | 2.92 | 3.46 |
| 22:00 | 5758 | Modena vs US Ancona 1905 | 1.43 | 4.40 | 7.00 |
| 23:00 | 2876 | CA Atlanta vs Flandria | 2.43 | 2.77 | 3.06 |
| 23:05 | 4319 | Defensores Belgrano vs Nueva Chicago | 1.99 | 3.02 | 3.75 |

JUMANNE - 29/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:00 | 3815 | Botafogo SP vs Inter De Limeira SP | 2.01 | 3.12 | 3.56 |
| 01:00 | 5254 | Ituano SP vs EC Agua Santa SP | 1.85 | 3.30 | 3.88 |
| 01:10 | 4280 | Instituto Cordoba vs Ferro CO | 2.44 | 2.88 | 2.92 |
| 01:30 | 1163 | Deportivo Pasto vs La Equidad | 2.24 | 3.02 | 3.11 |
| 02:00 | 3138 | Agropecuario vs Independiente Rivadavia | 2.32 | 2.92 | 3.07 |
| 02:00 | 5111 | Atletico Rafaela vs Deportivo Madryn | 2.18 | 2.91 | 3.35 |
| 02:30 | 3093 | Santamarina vs Deportivo Moron | 2.86 | 2.77 | 2.57 |
| 13:35 | 5417 | Japan vs Vietnam | 1.11 | 7.01 | 17.54 |
| 14:00 | 2187 | Gibraltar U21 vs Moldova U21 | 10.71 | 5.84 | 1.20 |
| 14:00 | 4271 | Kazakhstan U21 vs Scotland U21 | 4.39 | 3.86 | 1.63 |
| 14:30 | 4068 | Iran vs Lebanon | 1.29 | 4.57 | 9.33 |
| 14:35 | 1381 | Gokulam Kerala FC vs Rajasthan United | 1.91 | 3.02 | 4.09 |
| 16:45 | 1603 | United Arab Emirates vs South Korea | 3.97 | 3.39 | 1.81 |
| 16:45 | 2712 | Syrian Arab Republic vs Iraq | 3.44 | 2.86 | 2.17 |
| 17:00 | 2485 | Kazakhstan vs Moldova | 2.20 | 2.95 | 3.60 |
| 17:00 | 3516 | Croatia vs Bulgaria | 1.45 | 4.16 | 7.71 |
| 19:00 | 1914 | Oman vs China | 1.81 | 3.25 | 4.18 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Machi 28, 2022
Nipashe





## Rashford aingia anga wanaosakwa Arsenal

VITASA!...



Bondia Twaha Kassim 'Kiduku' (kushoto), akijipanga kumsukumia konde mpinzani wake, Alex Kabangu kutoka DR Congo, katika pambano la raundi nane lililopigwa usiku wa kuamkia jana mjini Morogoro na Kiduku kushinda kwa pointi. **MPIGAPICHA WETU**

# PABLO ATANGAZA SIKU 7 ZA JASHO SIMBA CAF

●●●Asema zinatosha kuiua Gendarmerie, nyota wote kambini, TFF yaruhusu waliopo Stars...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amesema siku saba alizonazo za kukinoa kikosi chake kabla ya mchezo wa mwisho wa hatua ya makundi dhidi ya US Gendarmerie ya Niger, zinamtosha kuhakikisha wanapata pointi tatu na kufuzu hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kikosi cha Simba kimeingia kambini jana tayari kwa maandalizi ya mechi dhidi ya Gendarmerie ambayo itaamua hatima yake ya kufuzu robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika ama la.

Katika mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumapili wiki hii, matokeo ya ushindi pekee ndio yatakayoiwezesha Simba kufuzu hatua ya robo fainali.

Hiyo ni kutokana na Kundi lao la D, Asec Mimosas kuwa kileleni ikiwa na pointi tisa huku RS Berkane na Simba zote kila moja ikiwa na alama saba huku US Gendarmerie ikiburuza mkia na pointi zake tano, hata hivyo timu zote katika kundi hilo zina nafasi ya kufuzu robo fainali.

Sare yoyote kwa Asec Mimosas itakuwa imekata tiketi ya robo fainali huku RS Berkane ambayo itakuwa mwenyeji katika mchezo wa mwisho dhidi ya Waivory Coast hao, ikilazimika kushinda ili kufuzu hatua inayofuata.

Lakini kama Simba ikipoteza na Asec Mimosas ikaifunga RS Berkane, basi miamba hiyo ya Ivory Coast na US Gendarmerie zitafuzu robo fainali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Pablo alisema wamerejea kambini na watakuwa na wiki moja ya kukimbizana na anaimani kwamba itatosha kushinda mechi hiyo yenye umuhimu mkubwa kwenye soka la Tanzania.

Alisema siku ni chache za kufanya maandalizi mazuri lakini wanaamini zinatosha kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo huo.

"Baada ya kurejea kambini tutakuwa na wiki moja hivi ya kufanya maandalizi, ninaimani inatutosha kwetu na kwa kila mchezaji kufanya kile kinachohitajika katika kufanya vizuri kwenye mchezo dhidi ya Gendarmerie," alisema na kuongeza;

"Malengo yetu makubwa ni kufuzu katika hatua inayofuata kutokana na kiu ya mafanikio tuliyokuwa nayo, ninaimani kubwa hilo linawezekana ingawa tutakuwa na mechi ngumu kutokana na wapinzani wetu nao wananafasi kama sisi," alisema Pablo.

Alisema ana matarajio makuwa na kikosi cha timu hiyo kufanya vizuri katika uwanja wa nyumbani.

Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema wachezqji waliokuwa wameitwa kikosi cha timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) nao watajumuika kikosini baada ya kuombewa ruhusa kwa uongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania, TFF.

Alisema Peter Banda ambaye aliitwa Timu ya Taifa ya Malawi naye ameombewa ruhusa ya kutoenda kujiunga na timu yao, hivyo ni miongoni mwa wachezaji walioingia kambini.

"Hadi sasa hakuna mchezaji majeruhi, hivyo wote waliosajiliwa kwa ajili ya mashindano ya CAF wataingia kambini leo (jana) tayari kwa maandalizi ya mchezo wetu dhidi ya US Gendarmerie," alisema.

"Mchezo huu tumeupa umuhimu mkubwa na tunauchukulia kama fainali kwa sababu ni ushindi tu ndio utatupa nafasi ya kutinga robo fainali," alisema Ahmed.

Wakati huo huo CAF imeruhusu mashabiki 35,000 katika mchezo huo ingawa Simba walitamani kuongezewa idadi kubwa zaidi kulingana na umuhimu wa mechi hiyo.

Alisema tiketi zimeanza kuuzwa tangu juzi kwa njia ya mitandao ya simu, hivyo mashabiki wanapaswa kununua mapema ili kuepuka usumbufu siku ya mchezo.

## Kabangu: Kiduku? Mwakinyo kiboko

**Saada Akida na ShufaaLyimo**

LICHA Bondia Mtanzania, Twaha Kassim 'Kiduku', kushinda kwa pointi dhidi ya Alex Kabangu kutoka DR Congo, Mkongomani huyo amesema kwake Hassan Mwakinyo ndiye bondia bora zaidi kwa hapa Tanzania.

**UK. 20**

## Nigeria vs Ghana vitani Qatar 2022



**ABUJA, Nigeria**

UKITAJA mchezo kati ya Nigeria dhidi ya Ghana, kwa wengi yatakuja mambo mawili makubwa - ushindani wa hali ya juu kwenye soka na chakula kinachoitwa 'Jollof rice', (pilau) ambacho ni maarufu Afrika.

**UK. 11**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >